# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 25 Aprili, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:-**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo ni siku nyingine ya Alhamisi Maswali kwa Waziri Mkuu tunao waliomba kama tisa bila kumjumuisha Kiongozi wa Kambi ya Upinzani. Mkiuliza maswali yenu kwa kifupi tunaweza kufikia idadi kubwa zaidi. Sasa namwita Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, aanzishe mjadala huu.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kwanza ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, maji ni jambo ambalo ni la msingi mkubwa mno kwa sababu linagusa Watanzania wote kwa maana ya Watanzania karibu milioni 45, na maji katika nchi yetu yanasimamiwa na Sera ya Maji ya mwaka 2002 sambamba na Sheria ya Maji ya mwaka 2009; na kwa sababu pameonekana kwamba kuna uzito mkubwa wa kutekeleza ahadi pamoja na Sera ya Maji; na kwa sababu Wabunge walio wengi wame-*complain* kwa kiwango kikubwa mno kwamba hapajatolewa fungu la kutosha kuiwezesha Wizara ya Maji kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sera ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni kwa nini sasa pengine Serikali isione umuhimu wa kuondoa mjadala wa maji unaoendelea katika Bunge hili kwa sasa ikafikirie upya namna ya kutengeneza fungu maalum ambalo litawezesha maji kweli kutumika kama *resource* ambayo itawasaidia Watanzania mamilioni ambao wanateseka kwa ajili ya kukosa maji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu maelezo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, maji ni suala muhimu kwa Watanzania lipo wazi na mimi ninakubali kabisa, na ndiyo maana kama Serikali tunafanya juhudi kulingana na uwezo wa kifedha uliopo kuona ni namna gani tunaweza kuwa tunakabiliana na tatizo hili la maji. Kwa hiyo, hata ule

mradi ambao mliona tuliuibua kutokana na msaada wa fedha kutoka Benki Dunia ilikuwa ni kwa nia njema ya kujaribu kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nataka tu nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba kama Serikali jambo hili tunalijua na ndiyo maana tunajitahidi kufanya kila tunaloweza. Tatizo ni la kibajeti, tatizo zaidi ni uwezo wa kifedha. Tulipowasilisha hapa Bajeti ya Kilimo, Chakula na Ushirika wote mlisema Bajeti haitoshi na mimi nina hakika katika Sekta zote zinazokuja mtasema Bajeti hazitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tatizo ni udogo wa kiasi cha fedha ambacho inabidi tugawane katika kujaribu kukidhi mahitaji ya Sekta zote ambazo ni muhimu. Sasa rai yako ni nzuri, lakini sina hakika kama pengine huo ndiyo utakuwa utaratibu muafaka kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoweza kumwomba na kuliomba Bunge, maadam kwa utaratibu wa Kanuni za sasa umetoa fursa nzuri ya siku kama sita kwa Serikali baada ya kuwa tumepokea maoni ya Wabunge kutazama ni namna gani tunaweza tukaboresha baadhi ya maeneo kulingana na maoni na ushauri wa Wabunge.

Pengine hilo lingekuwa jambo muafaka zaidi na mimi kama Kiongozi wa upande wa Serikali tumeishaanza kulitazama tunajaribu kuona namna gani tunaweza angalau tukaokoteza okoteza fedha kutokana na fedha zinazotokana hasa na upande wa *OC* kwenye matumizi ya kawaida kupunguza katika baadhi ya maeneo ili tuweze kuongeza kiasi fulani cha fedha katika eneo hilo la maji.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru kwa majibu yako ambayo ni ya msingi sana.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu utakubaliana na mimi kwamba kupanga ni kuchagua. Ni kweli Sekta mbalimbali katika nchi yetu zinahitaji msukumo wa kibajeti, lakini ni ukweli vilevile kwamba jambo la maji na suala la maji ni *priority.*

Mimi nina imani kabisa hata katika kilimo kama hatutakuwa na utawala maalum wa Sekta ya Maji katika kukisaidia kilimo hatutaweza kuuondoa umaskini wa wananchi wetu.

Pamoja na kwamba maji yanatumika zaidi kwa matumizi ya binadamu kama *first priority,* lakini vilevile maji yanastahili kutumika kama *resource* muhimu sana katika masuala ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini kwa wananchi wetu.

Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu umekiri kwamba Serikali itaangalia uwezekano wa kuongeza Bajeti ya Maji na Bunge lisaidie katika upande huo.

Vilevile tunatambua maji ni *finite resources* yaani ni rasilimali inayokwisha na Sera ya Maji ya mwaka 2002 haijabainisha kwa undani matumizi ama *factor* ya kuvuna maji ya mvua kama sehemu muhimu katika *Water Resource Management*.

Je, Serikali itakiri kwamba katika marejeo hayo ya Bajeti ya Wizara ya Maji itaweka vilevile kipaumbele katika suala la uvunaji wa maji ya mvua kama sehemu ya kukuza rasilimali maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu maelezo.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, katika jitihada hizi za Serikali suala la uvunaji wa maji ya mvua ni sehemu ya utaratibu au mradi ambao Serikali tunakwenda nao. Mtaona katika baadhi ya maeneo ambayo tumeibua uchimbaji wa mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua *component* moja ni matumizi ya binadamu, lakini nyingine ni mifugo, lakini nyingine vilevile tumeitumia kwa ajili ya umwagiliaji.

Kwa hiyo, ni eneo moja tunalitambua ni muhimu sana na tunakwenda nalo kwa sababu tunajua ni eneo ambalo lazima tulizingatie.

Lakini tutakapokuwa tunatazama hili ambalo ni la sasa tutakachoona kwanza ni kiasi cha fedha tutakachoweza kukipata, halafu tuone ni maeneo yapi ambayo pengine yapewe nafasi katika Bajeti hii kulingana na kiasi ambacho tutakuwa tumepata. Kwa sasa kilio kikubwa ni mahitaji ya maji kwa matumizi ya binadamu hasa vijijini kwa sababu bado kunahitajika *effort* kubwa zaidi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kama ninaweza kupata fedha za kuwezesha kupata maji kwa Watanzania vijijini nitaweka umuhimu mkubwa sana katika eneo hilo kwa sasa kwa kutumia vyanzo vyovyote vile tutakavyoweza kuvipata katika ngazi ya vijiji. Kwa hiyo, tutaangalia tuone ni kiasi gani tutaweza tukiwa na fedha za kutosha wazo lako siyo baya hata kidogo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tumechukua dakika kumi. Sasa naomba mnaokuja msije na hotuba ndefu ili kusudi tuweze kupata idadi kubwa. Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa Watanzania wamekubali kuondoka kwenye matumizi ya *analogue* na kujiunga na matumizi ya *digital* kwa kununua ving'amuzi na bei ya kununulia ving'amuzi ilikuwa ni shilingi 39,000 lakini sasa hivi ving'amuzi hivi vimefikia shilingi 79,000 bei ambayo ni kubwa sana, Watanzania walio wengi wanashindwa kununua ving'amuzi hivyo.

Je, Serikali ipo tayari kufuatilia zoezi hili na kuona namna ya kuzungumza na Mashirika haya kwa lengo la kuwasaidia Watanzania ili ipatikane bei ambayo kila Mtanzania atamudu kununua ving'amuzi hivi? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nipokee ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tutampa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia suala hilo alitazame, na nafikiri atakuwa na maelezo pengine mazuri zaidi wakati wakiwasilisha Bajeti yake.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa baada ya kununua ving'amuzi hivi bado Mtanzania anaendelea kununua *channel* kwa kila mwezi, anayehitaji *channel* chache anatoa shilingi 9,000 na mwingine mwenye kuhitaji *channel* nyingi kidogo anatoa shilingi 18,000 na mwenye kuhitaji *channel* nyingi zaidi anatoa shilingi 36,000; kwa kuwa watanzania wote wanahitaji hizi *channel* zote.

Je, katika mazungumzo hayo Serikali itakuwa tayari kuangalia *channel* zitolewe zote kwa Watanzania na itolewe bei ambayo kila Mtanzania atanunua *channel* hizo zote?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema eneo hili kidogo linahitaji maelezo ya wataalam zaidi si la kisera sana. Kwa hiyo, ndiyo maana naomba nilipokee tu huo ushauri Wizara ya Kisekta inayohusika ili iweze kupata nafasi ya kutoa maelezo ambayo ni fasaha zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya kutunga Sheria katika jamii yoyote duniani ni kuondoa kero ambazo jamii inaizunguka. Katika nchi yetu na kupitia Bunge hili Tukufu tulitunga Sheria ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani, Sheria hii badala ya kuondoa kero kwa wakulima hasa wa korosho imeongeza kero. Hivi karibuni tumeona vuruga nyingi zikitokea na watu wengine ambao hawana nia njema katika nchi yetu wamekuwa wakitumia kisingizio hiki cha Sheria ya Stakabadhi Ghalani kuleta vurugu.

Je, Serikali haioni sasa hivi ni muda muafaka wa kuiangalia sheria hii haraka iwezekanavyo na ikibidi waisimamishe kwa misimu hii miwili mfululizo ili wakulima wa korosho waweze kunufaika na zao lao la korosho? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuliwasilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Stakabadhi Ghalani na ilipitishwa na kama mtakumbuka lengo kubwa kabisa la Sheria lile ilikuwa ni dhamira njema ya Serikali ya kuona namna nzuri ya kumkinga au kumlinda mkulima huyu hasa kutokana na bei ambazo wakati mwingine wanunuzi walipokwenda vijijini wananunua bidhaa mbalimbali kwa bei ya chini sana. Kwa hiyo, ilikuwa lengo kwamba tuwe na utaratibu ambao utawezesha wakulima kuwa na kauli ya bei zao kwa maana ya kupanga bei na mtu akanunue kutoka katika vituo mahsusi ambavyo vimetengwa.

Sasa tunatambua kwamba inawezekana katika jambo hili kwa sababu linahitaji fedha na wakati mwingine inabidi kukopa benki inaweza kuwa imeleta tatizo katika utekelezaji wa Sheria yenyewe. Lakini bado nataka nisisitize kwamba nia ni nzuri. Mara ya kwanza nilipokwenda Mtwara kukumbana na jambo hili nilikuta korosho kilo moja walikuwa wanainunua kutoka kwa wakulima kwa shilingi 50, iliniuma sana sana. Ndiyo maana tukafikiria kwamba pengine namna bora ni hiyo. *(Makofi)*

Sasa kama yapo matatizo Serikali itayaangalia na tutashirikiana kujaribu kuona namna gani tunaweza tukaondoa kero hiyo na pengine kuiweka katika mazingira ambayo yanaweza kuwa ni muafaka zaidi. Lakini bado tujaribu kumlinda mkulima kwa kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA A. MTURURA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Lakini moja ya kero ambazo zinaletwa na mfumo huo wa Stakabadhi Ghalani ni kuzaliwa kwa tozo mbalimbali ambazo zinazalishwa na Vyama vingi vya Ushirika pamoja na Taasisi mbalimbali za Kiserikali.

Je, katika mfumo huo mpya ambao sasa hivi inauangalia Serikali itakuwa tayari kutoa amri ya kuondoa tozo hizi ambazo zina lengo la kumnyonya mkulima wa korosho? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Mtutura Abdalla Mtutura, ni kweli na ni jambo la lazima tuliangalie. Kwa sababu ukichukua mfano wa korosho tu zipo tozo kumi kutoka Taasisi na vyombo mbalimbali na ukijumlisha kiwango cha fedha ambazo zinatozwa kwa kilo moja ya korosho ni shilingi 220.

Kwa hiyo, mkulima anakosa kiasi kikubwa cha fedha ambazo zingeweza kumrudia yeye na nyingine kusema kweli hazina sababu. Nyingine ni mambo ya Bodi, Bodi wanailipa kwa nini kwa sababu Bodi tunaigharamia Serikali, Vyama vya Msingi, Vyama vya Ushirika, wapo *transporters* pale. Ni kweli wamejenga taratibu ambazo unaweza ukasema ni za kujinufaisha zaidi kuliko za kumsaidia mkulima. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kimsingi tumelikubali na tumeishaanza kulifanyia kazi na ndiyo maana Waziri wa Kilimo aliahidi Bunge lako Tukufu hapa kwamba tutafanya kila litakalowezekana kukaa na wadau na kuondoa baadhi ya maeneo ambayo tunaona kwa kweli hayastahili. Siyo korosho tu, mifumo hii utaikuta kwenye tumbaku, utaikuta kwenye pamba na ndiyo maana unakuta wakati mwingine inaleta zogo kubwa sana kwa sababu ya utaratibu ambao mifumo hiyo imeweka.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Tanzania ni moja kati ya nchi kumi ambazo zinazalisha mkaa kwa wingi duniani ambapo asilimia 3 ya mkaa wote unaozalishwa duniani unatoka Tanzania kiasi cha kwamba takriban ya tani milioni moja tunazalisha kwa mwaka ni sawa na tani 2650 kwa siku ambazo tunazalisha Tanzania.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, tani hizi ambazo tunazalisha Tanzania zinasaidia katika uchumi wa Taifa takriban *dollar* milioni 650.

**SPIKA:** Naomba swali liwe fupi.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Je, Serikali yako ina mustakabali gani wa kisheria na kisera kuwatambua na kuwaendeleza wazalishaji hawa ambao ni wananchi wa kawaida wa vijijini na wale ambao kwa kweli kipato chao ni duni?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kueleza suala hili ambalo Mheshimiwa Rajab ameliuzia. Mwanzoni nilipata tabu maana sikujua kama ni mkaa wa mawe au ni mkaa unaotokana na kuni. Kumbe ni mkaa unaotokana na miti, misitu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, analolisema ni kweli kwamba Tanzania ni moja ya nchi ambazo tunatumia mkaa unaotokana na ukataji misitu kwa kiwango kikubwa sana. Tunaweza tukadhani ni neema lakini kwa kweli ni changamoto kwa upande wa Taifa letu. *(Makofi)*

Ni changamoto kwa sababu ukataji ule unachangia sana katika uharibifu wa misitu. Jambo ambalo lina athari kubwa sana kama Taifa, lakini kama ulimwengu vilevile. Sasa wakati ninakubaliana na wewe kwamba hiyo ndiyo hali ilivyo sasa si jambo ambalo ningependa kama Serikali tukataka tulihimize na kuliendeleza la hasha. Hatutakuwa tumefanya uamuzi wa busara.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri la kukubaliana hapa kama Serikali na kwa Watanzania tuone ni mambo gani mbadala ambayo mwananchi huyu anaweza akafanya na yakamwezesha kupata kipato chake.

Lakini wakati huo huo tujibu ni nini mbadala sasa ambacho mwananchi atatumia kama nishati hasa Mijini. Ndiyo maana tunashukuru kwamba Serikali kwa jitihada zake sasa tuna fursa kubwa ya gesi. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba tukijipanga vizuri, gesi hii itatusaidia sana katika matumizi ya nyumbani na hivyo tutapunguza kwa kiasi kikubwa matumizi ya ukataji wa misitu kwa ajili ya nishati ambayo mimi nadhani haitupeleki mahali pazuri sana. (*Makofi*)

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inajipanga na tunasubiri manufaa ya hii gesi familia takribani milioni moja nchini zinategemea mauzo haya au uzalishaji huu wa mkaa. Je, Serikali ina tamko gani kwa sasa hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukapike na huko nyumbani.

**WAZIRI MKUU:** Naona Mheshimiwa bado anataka tuseme tunatoa baraka kwa hayo, hapana. Mimi nafikiri tusitoe baraka za namna yoyote ile tutaendelea kujaribu kutumia sheria tulizonazo sasa na Kanuni tulizonazo sasa kwamba ukataji wa misitu kwa ajili hiyo nao udhibitiwe, usimamiwe usiwe holela maana tukiliachia hilo likawa holela kama ninavyosema ni tishio kubwa sana kwa Taifa letu mnaweza unatishia nchi yenu kuwa jangwa kama vile hamkuwa mnajua tatizo lenyewe.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hivi karibuni baadhi ya Wabunge wamegeuka kuwa kama wasemaji wa Serikali wanapokuwa kwenye Shughuli za Bunge hapa Bungeni na hivyo kuweza kulifanya Bunge letu kuweza kupoteza mwelekeo katika suala zima la kuishauri na kuisimamia Serikali ipasavyo.

Je, Serikali yako iko tayari kuweza kutunga sheria ambayo itazuia Wabunge kutokuwa wasemaji kama ambavyo imejijengea kama ni utamaduni wetu?

**SPIKA:** Utamaduni gani? Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, namwomba arudie maana swali lake naona sijamwelewa hata kidogo.

**SPIKA:** Halieleweki

**MHE. MOSES J. MACHALI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru Serikali iko tayari kuweza kutunga sheria ya kuzuia baadhi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamegeuka kuwa wasemaji, washauri au wasemaji wa Serikali tunapokuwa kwenye vikao vyetu vya Bunge na hatimaye sasa Bunge letu linapoteza mwelekeo katika suala zima la kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali ipasavyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ni kweli.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina hakika kama kweli unahitaji sheria kwa jambo hili. Kwa sababu kama wewe unajifanya kuwa ni msemaji wa Serikali unataka nikutungie sheria ya kukuzuia usifanye hivyo, mimi nafikiri hapana. Nadhani rai nzuri ingekuwa kutoa wito kwa Wabunge wote kwamba katika kuishauri Serikali tuzingatie Kanuni zetu za Bunge maana Kanuni zile zimewekwa kwa ajili ya kutusaidia sisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwamba utahitaji sheria mahsusi kwa jambo hili, mimi sidhani. Lakini ni kweli kabisa kwamba wakati mwingine na mimi napata taabu kidogo na hasa yanapokuwa mambo yametokea hapa Bungeni au pengine kwenye Kamati, lakini wakati mwingine hata halijafikia tamati lakini utamwona Bwana Machali yuko kwenye majukwaa huko analisemea na kadhalika. Sasa wakati mwingine nalo si zuri sana. Ndiyo maana nilikuwa nafikiri kwamba kubwa ni kurudi kwenye Kanuni tukizifuata zimewekwa vizuri sana zitatusaidia sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ndio Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa nafasi yako una mamlaka na wajibu wa kuhakikisha Serikali inatekeleza Maazimio ya Bunge.

Mwezi Novemba, 2011 Bunge lilipitisha Maazimio baada ya kufanya uchunguzi juu ya matumizi mabaya ya fedha kwenye Wizara ya Nishati na Madini, kwa taarifa ambayo iliitwa maarufu kama Sakata la Jairo.

Toka wakati ule mpaka hivi leo umepita mwaka mmoja na nusu Serikali haijawasilisha ndani ya Bunge hili taarifa ya utekelezaji wa Maazimio yaliyotokana na taarifa ile ya Kamati Teule na wala waliotakiwa kuchukuliwa hatua za kisheria hawajachukuliwa hatua za kisheria mpaka hivi leo. Ni kwa nini Serikali yako imekuwa ikidharau kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa wakati?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli hiyo ni sehemu ya jukumu langu na jitihada zinafanyika kila tunapopata ushauri wa Wabunge tunayafanyia kazi hatuyapuuzi hata siku moja. Kwa hiyo, hata hili pengine ungeweza tu kusema kwamba Bwana Mheshimiwa Waziri Mkuu lini utatuletea taarifa ya utekelezaji juu ya jambo hili na tutafanya tu hivyo kwa sababu si kwamba hakuna kilichofanyika.

Tumeshachukua hatua kadhaa ambazo ndani ya Serikali pengine kilichokosekana sasa ni kurejesha mrejesho nini mpaka sasa tumejaribu kufanya na kipi bado hatujakamilisha. Hilo nafikiri halina tatizo. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni lini utaleta Bungeni taarifa ya utekelezaji wa hayo Maazimio yote?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, wakati wowote kuanzia sasa. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali ilikuwa na nia njema ya kudhibiti matumizi yake kwa kufanya manunuzi kwa kupitia zabuni.

Lakini uhalisia uliopo katika maeneo mengi ni kwamba bidhaa zinazonunuliwa kwa wazabuni zinakuwa za bei ya juu kuliko bei ya kawaida na hata kama ni majengo yanayojengwa kwa zabuni yanakuwa na bei ya juu kuliko bei ya kawaida na wakati mwingine yanakuwa na bei ya juu wakati kiwango ni cha chini kuliko vya kawaida.

Je, Serikali inatoa kauli gani na itakuwa tayari kurekebisha kuleta Muswada ili kurekebisha kasoro ambazo zimejitokeza?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, lengo la sheria ile ilikuwa ni kuimarisha dhana ya uwazi katika usimamizi wa shughuli ya manunuzi, ilikuwa hasa ndio dhamira yake na ndio maana katika sheria ile utaona uko mfumo umewekwa wa kutangaza baadaye mnawasaili mnapata mtu ambaye mnafikiri ana sifa stahiki huyo ndiye mnayempa kazi ya kufanya.

Kama mtakavyokumbuka ndani ya sheria ile imewekwa bayana kwamba yule atakayekuwa ametoa bei ya chini kutegemea na aina ya zabuni ilivyo basi huyo ndiye tutakayempa nafasi ya kwanza ama yule atakayetupa bei ambayo ni ya juu zaidi kutegemea na aina ya zabuni huyo ndiye tutakayempa nafasi ya kwanza.

Kwa hiyo, dhamira yake ilikuwa ni nzuri sana. Tatizo lililopo hapa sasa ni uaminifu wa wasimamizi na watendaji ambao ndio wanaotumia ile sheria vibaya na hili jambo ni changamoto kubwa sana. Kwa hivyo kama anavyosema Mheshimiwa Mwigulu nadhani tukubali kwamba pengine kuna haja ya kuitazama sheria ile tuone kama kwa namna tulivyokuwa tumeitunga hapa Bungeni kwamba iliweza kweli kuziba mianya yote ambayo inampa fursa mtu mwingine kuitumia vibaya.

Lakini si hiyo tu, liko tatizo vilevile la kucheleweshwa sana na mlolongo mrefu sana kabla hamjafikia hatua ile ya mwisho. Pengine nalo hili itabidi tuliangalie tuone namna gani tutashughulika na jambo hili. Upande wa Serikali

tulikwishaanza tayari timu ndogo ambayo inalifanyia kazi nadhani tutakapokuwa tumekamilisha tutawasilisha baadhi ya mawazo ambayo tunajaribu kuyapata ili Bunge nalo liweze kutusaidia kutupa mchango zaidi. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Waziri Mkuu tatizo la msongamano katika miji mikuu hasa Dar es Salaam imekuwa ni kero na ni gharama kubwa kwa maisha

**SPIKA**: Msongamano wa nini?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU***:* Msongamano wa magari katika barabara ni tatizo kubwa na sasa limeongezeka linasababisha ajali nyingi sana kwa askari wa usalama barabarani. Ili kuondoa hili ni lini Serikali itanunua helikopta ili kuondoa kero ya misafara ya viongozi ambayo inakwamisha magari kila wakati?

**WAZIRI MKUU**: Mheshimiwa Spika, nina hakika kabisa siku tukinunua helikopta kwa ajili hiyo Bunge lote mtatugeuka hapa. Wote mtageuka. *(Makofi)*

Naelewa analolisema Mheshimiwa Mangungu, sitakubaliana naye sana kwamba suluhu ni sisi akina Pinda kununua mahelikopta ya mabilioni tuanze kuruka kwa sababu sisi labda ndio tunasababisha misafara na kadhalika na kadhalika hapana.

Mimi bahati nzuri napata nafasi ya kutembea nchi nyingi, viongozi wote wanatumia barabara hizi hizi na ni suala la utaratibu tu wa namna nzuri ya kuwezesha viongozi kupita na upande mwingine kuhakikisha kwamba askari wetu wako salama.

Yako mambo mawili ambayo nayaona. Moja ni mfumo tuliojiwekea wa namna ya kuwezesha viongozi kupita wakati ule ule kuwezesha magari mengine kupita. Ukienda hata Kenya kiongozi unaingia kwenye msafara lakini magari mengine yote yanaruhusiwa kuendelea na safari zake.

Mnapishana kubwa tu ni wewe ambaye unaongoza msafara wa kiongozi ili msije mka-*create* msongamano ambao siyo wa lazima sana. Kwa sababu kinachotokea wakati mwingine mnapokuwa mmesimamisha magari linapomalizika gari moja unapoachia magari mengine kuanza kuingia wakati mwingine ndio kunatokea mtafaruku ambao sio wa lazima sana.

Sasa tunaendelea kujaribu kuzungumza na wenzetu wa Polisi pamoja na vyombo vya usalama kuona namna nzuri zaidi ya kuweza kuwapitisha viongozi hawa bila kulazimisha pengine msongamano mkubwa ambao baadaye unaleta tatizo katika kuwapisha watu wengine kuweza kupita salama. Kwa hiyo, ni changamoto lakini si kubwa tunaendelea kuitafutia ufumbuzi. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa majibu mazuri. Lakini gharama ya ununuzi wa helikopta ukiangalia tathmini iliyofanyika na wataalam wa usafirishaji kila siku sio chini ya shilingi bilioni 4 zinapotea kwa wananchi na watumaiji wengine wa barabara.

Sasa ili kuondoa tatizo inaweza ikawa Bunge litaingilia kati lakini ningependa Serikali yako sasa ichukue wajibu na jukumu la kufanya tathmini ipi ni gharama kubwa aidha kwa kutumia vyombo hivyo vya usafiri lakini pia kwa kipindi cha mpito itangazwe sasa ni misafara ipi ambayo inaruhusiwa kuzuia magari maana yake sasa hivi misafara imekuwa mingi. Waziri Mkuu yuko Dodoma, Rais yuko nje ya nchi bado unaona ving'ora vinaongezeka mitaani.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mangungu anatutakia mema lakini bado nafikiri wacha tulitazame jambo hili kwa upana wake maana inawezekana tatizo pengine ni msongamano kwa sababu barabara zetu ni nyembamba zinahitaji kuboreshwa zaidi.

Ule mradi ambao tunaozungumza wa Mabasi yaendayo kwa kasi, siyo kwamba tunataka tu watu wengi waweze kusafirishwa Dar es Salaam, lakini vilevile kuongeza upana wa barabara zetu ili kuruhusu magari mengi zaidi kupita kwa namna ambayo ni salama zaidi. Kwa hiyo, tunachanganya mambo mengi katika kujaribu kutafuta ufumbuzi wa jambo hili kwa pamoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha. Tukushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kujibu maswali na maswali kidogo yameenda kisekta zaidi kuliko yale ya kisera. Kwa hiyo, tujaribu kuendelea kuuliza maswali vizuri. Tunaendelea, Katibu!

## MASWALI YA KAWAIDA

Na. 105

### Wizara ya Ardhi, Elimu na Afya Kupelekwa TAMISEMI

**MHE. MOSSES J. MACHALI** aliuliza:-

(a) Je, ni sababu gani inayofanya Serikali kuweka usimamizi wa baadhi ya mambo yanayohusu Ardhi, Elimu na Afya chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na hivyo kuiongezea mzigo mkubwa?

(b) Je, ni lini Serikali itaondoa masuala ya Ardhi, Elimu na Afya kutoka TAMISEMI ili kupunguza urasimu katika utoaji huduma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, chimbuko la upelekaji wa Madaraka kwa Umma ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 katika ibara ya 8(1), 145 na 146.

Aidha, Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 ya mwaka 1982 (Mamlaka za Miji) ambazo zinatambua uwepo wa Mamlaka za Serikali za Umma kama vyombo huru vya kuwahudumia wananchi. Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma unazingatia misingi mikuu minne ambayo ni kupeleka madaraka ya kisiasa, rasilimali fedha, majukumu, na rasilimali watu kwenda kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako ndiko utekelezaji wa Sera na Mipango ya Kitaifa unafanyika. Lengo kuu ni kuimarisha na kusogeza huduma za jamii karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kupeleka masuala ya Ardhi, Elimu na Afya katika Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI unatokana na Katiba, Sheria na Sera ya Upelekaji wa Madaraka kwa umma ambayo inazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa madaraka na mamlaka ya kujiamulia mambo yao wenyewe kwa kujiletea maendeleo kwa kuzingatia matatizo yaliyopo. Serikali Kuu imebaki na jukumu la kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo mbalimbali na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizopo, utekelezaji wa Sera hii umekuwa na manufaa makubwa yakiwemo kupungua kwa tofauti za kimaendeleo kati ya Mkoa na Mkoa na Halmashauri moja na nyingine.

Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa umma ambayo ni sera mtambuka inayohusisha sekta zote zikiwepo Ardhi, Elimu na Afya kwa kuziimarisha Sekretarieti za Mikoa ili ziweze kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo niliyoyataja katika sehemu (a) hapo juu, ni dhahiri kwamba uendeshaji wa masuala ya Ardhi, Elimu na Afya utaendelea kutekelezwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Serikali Kuu itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufuatilia kuona kwamba malengo ya kuhamishia utekelezaji wa masuala yanayohusiana na utoaji huduma kwa wananchi yanafanikiwa. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nimwuliza maswali madogo mawili madogo ya nyongeza.

Kutokana na majibu mbalimbali ambayo yamekuwa yanatolewa na Mawaziri wa Serikali yetu imedhihirisha wazi kwamba sehemu kubwa huwa wanatupia mzigo TAMISEMI katika suala zima la kuweza kufanya maamuzi na hivyo kudhihirisha kwamba kauli ambayo imetolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri ya kwamba Serikali kuu imebaki na jukumu la kutunga na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo hiki kitu hakipo.

Je, Wizara yako chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haioni kwamba ipo haja ya kuhakikisha kwamba sasa inawapatia mamlaka Mawaziri wa Wizara nyingine kama za Ardhi, Elimu na nyinginezo ili kuhakikisha kwamba zinakuwa na uwezo au mamlaka ya kutosha tofauti na ilivyo hivi sasa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, inaeleweka bayana kwamba sheria hizo umezitaja lakini sheria sio Msahafu kama ilivyo Biblia na kadhalika. Wizara yako inaweza ikawa tayari kufanya mabadiliko ili kuhakikisha kwamba sasa Wizara zote zinaweza kuonyesha uwezo na hivyo kuwa na tija kwa wananchi katika suala zima la kushughulikia mambo mbalimbali yanazihusu Wizara hizo ambazo ziko chini ya TAMISEMI?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hili ambalo Mheshimiwa Moses Machali analizungumzia hapa sio mara yake ya kwanza analizungumza. Amewahi kuja mpaka ofisini, nimekuja na hii sheria hapa na nilimwonyesha Katiba ya Nchi inasema nini. Kwa kweli akasema kwamba siyo Msahafu. Labda tuwe *concrete* tueleze hapa kwamba nini kinachosemwa hapa.

Tulipoanzisha shule za sekondari katika Kata kwa maana hii anazungumza Mheshimiwa Machali ingemaanisha mambo yafuatayo kwamba Mkuu wa Shule aliyekuwa Muleba au aliyekuwa Kasulu atoke kutoka Kasulu aende Dar es Salaam kwenye Wizara ya Elimu kwenda kutafuta chakula cha watoto ndicho kinachosemwa hapa.

Mimi nataka tuelewane vizuri ili tuweze kufahamiana. *I want to be concret.* Hapa tunazungumza habari D by D (*Decentralization by Devolution)* na dunia nzima inasema peleka madaraka, mamlaka, peleka *resources* zote kwa wananchi kule waliko, leo unakuja unasema hivi kuanzia leo tutarudisha tena yale madaraka kule tuliko.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nataka niliambie Bunge lako Tukufu hapa katika Afrika nchi pekee ambayo inasifiwa kwa kuhakikisha kwamba inapeleka madaraka na inapeleka rasilimali kwa wananchi, Tanzania ni ya kwanza. Wamekuja *South Africa,* Kenya, Rwanda na Burundi wamekuja kujifunza hapa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hapa hii kelele yote tunayopiga hapa ya kusema peleka mamlaka na madaraka kule Siha, peleka kule Mtwara, Magu hiyo kelele kama tukisema leo tunarudi tena kulekule tulikotoka, maamuzi yafanyikie huko!

Mheshimiwa Spika, tunachosema, Halmashauri function yake ya kwanza ni kupitisha bajeti, *function* yake ya pili ni kupitisha Sheria ndogo, *function* yake ya tatu ni kutoa huduma muhimu kwa jamii. Hivi tulivyo sasa hivi na haya matatizo yanayozungumzwa hapa, tukisema turudi tena nyuma, utaleta urasimu mkubwa hapa, tutawa-*confuse* wananchi hapa.

Mheshimiwa Spika, *it is my opinion* kwa niaba ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba kama kuna matatizo na changamoto zinazojitokeza hapa, tuzilete tuzizungumze hapa. Lakini tusikubali asilani kwamba tunarudi tena nyuma kule tulikotoka, madaraka yanarudi kule. Wizara zibakie na mambo ya *quality control,* mambo ya sera na mambo mengine kama tulivyoeleza hapa.

Mheshimiwa Spika, namwalika Mheshimiwa Moses Machali na wale wengine wote wanaofikiri kwamba tunaweza tukaendelea, tuzungumze zaidi kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya. Nitamwita mtu mmoja tu, Mheshimiwa Soni.

**MHE. JITU V. SONI**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri aliyoyatoa. Nilikuwa nauliza: Je, kama masuala yote hayo ya ardhi, afya na elimu yako TAMISEMI, kwanini sasa hakuna ushirikiano na maelewano katika Idara zote hizo wakati wanapopanga na kutekeleza miradi mbalimbali? Inakuwa kila moja inajitegemea. Lini watakuwa na *coordination* ili mambo yaende vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba ujibu kwa kifupi tu. Maana muda hautoshi!

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Mawaziri wote walioko hapa wanafahamu, kila wakati tunapokuwa na jambo lolote linalohusu mambo ya

kisera tunakutana, kama linahusu mambo ya afya tunakutana na Waziri wa Afya tunakaa naye, anakuja na timu yake na sisi tunakuja na yetu ya TAMISEMI, tunazungumza wote kwa pamoja kuhusu mambo ambayo tunafikiri kwa pamoja tunataka.

Mheshimiwa Spika, huyu Waziri aliyeko sasa hivi anayezungumzia habari ya maji, tunakwenda Ofisini kwake na yeye anakuja Ofisi kwetu tunakuwa na vikao vya watu wa maji na sisi tunakuwa na vikao vya kwetu vya TAMISEMI. Wote tunashirikiana vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, kama kuna upungufu mtuambie tu kuna upungufu, lakini *to the best of my knowledge,* wakati wote tumekaa katika vikao, tumeshirikiana nao na ndiyo maana hata wakati wa kujibu maswali hapa wakati mwingine tunashirikiana. Kama ni barabara tunajibu wote kwa pamoja.

**SPIKA:** Tumetumia dakika kumi kwa swali moja. Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Yusuph Nassir ndiye atauliza swali hilo.

Na. 106

**Kero ya Maji Korogwe Mjini**

**MHE. YUSUPH A. NASSIR** aliuliza:-

Kumekuwepo na kero ya muda mrefu ya maji Korogwe Mjini ambapo Serikali ilitoa taarifa ya miradi ya maji ambayo mpaka sasa haitekelezeki:-

(a) Je, Serikali itaondoa lini kero hii ya maji kwa wananchi wa Korogwe Mjini?

(b) Je, Serikali itatenga fedha kiasi gani kwa ajili ya kutatua kero hii; kwani visima vya Benki ya Dunia vimeshindwa kukidhi matarajio ya haraka ya wananchi wa

Vitongoji vya Mahenge, Kwakombo, Mgambo, Kitifu na Iwengera?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mbunge wa Korogwe Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la maji Mjini Korogwe, Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya kazi za kubadili mabomba chakavu, kuongeza chanzo cha maji kwa kuchukua maji ya kutosha kutoka Mto Mashindei pamoja na kujenga chujio la kuchuja na kutibu maji.

Aidha, Wizara ya Maji katika mwaka 2013/2014 (chini ya fungu 49), imeuweka Mji wa Korogwe katika orodha ya Miji ambayo ujenzi wa miradi ya maji inayoendelea utaharakishwa ili kuwapatia wakazi wake ufumbuzi wa dharura wa matatizo ya maji. Wastani wa Shilingi milioni 200 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeendelea kutekeleza miradi ya vijiji 10 katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe. Miradi hiyo inatekelezwa katika vijiji viwili vya Kwamndolwa na Kwameta ambayo itakamilika mwezi Juni, 2013.

Aidha, zabuni za kuwapata Wakandarasi wa ujenzi katika vijiji vitatu vya Kwakombo, Kwasemagube na Kwamsisi ambavyo ni vijiji vya nyongeza zimetangazwa. Vijiji sita vya Mgambo, Mgombezi, Kitifu, Mahenge, Msambiazi na Lwengera Relini vitatekelezwa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Kiasi cha Shilingi milioni 343.65 kimetengwa ili kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe.

**SPIKA:** Ahsante. Swali la nyongeza Mheshimiwa Nassir!

**MHE. YUSUPH A. NASSIR**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa suala la maji au tatizo la maji Korogwe Mjini lilikuwa pia ni sehemu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini kadhalika makuzi ya Mji wa Korogwe ni miongoni mwa Miji inayokua kwa kasi sana; na kwa kuwa pia siyo mara kadhaa tumekuwa tukizungumza hapa Bungeni kuhusiana na kadhia ya maji; na kwa kuwa katika michango ya maji na tukiendelea kuchangia bajeti, vyanzo mbalimbali vya mapato vimeshauriwa na Waheshimiwa Wabunge; na kwa kuwa kiasi cha pesa kilichotengwa kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kinaonekana ni kidogo, ni sawa na kumpa pipi mtu mwenye njaa ya miaka mitatu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza kabisa tatizo la maji Korogwe Mjini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli lipo tatizo kubwa la maji katika Mji wa Korogwe, nami nilipata nafasi ya kutembelea pale. Lakini vilevile tutambue kwamba tunayo bajeti finyu ambayo imepelekea tupate fedha kidogo katika Mji huu wa Korogwe. Niseme tu kwamba, tunayo Miji mingi, Miji midogo na Miji Mikuu ya Wilaya ambayo inazidi zaidi ya 132.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, tumeupa kipaumbele Mji wa Korogwe hata kwa kiwango kidogo tuanze kutekeleza hii miradi. Lakini hapo tutakapopata fedha za kutosha, Mji wa Korogwe utapewa kipaumbele ili tuweze kujenga miradi mikubwa kwa kutumia vyanzo vya maji ambavyo nimeviainisha.

**SPIKA:** Tunaendelea, kwa sababu suala lenyewe lipo kwenye mpango. Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuuliza maswali mengi. Mheshimiwa Esther Matiko swali linalofuata.

Na. 107

**Mradi wa Uchimbaji Bwawa Kata ya Nyahongo**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Wananchi wa Rorya wamekuwa na mahitaji makubwa ya bwawa na Serikali ilisharidhia kuchimba bwawa katika Kata ya Nyahongo na kwamba kati ya mwaka 2006 - 2009 Serikali imekuwa ikiweka suala hili kwenye bajeti yake kabla ya kuliacha miaka ya hivi karibuni bila utekelezaji wowote:-

Je, ni sababu gani zilipelekea kuondolewa kwa suala hili kwenye bajeti wakati hakuna utekelezaji wowote uliofanyika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mpango wa Ujenzi wa Mabwawa katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 iliweka bwawa la Kanyisambo katika bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Bwawa hilo lilipangwa kujengwa katika Kijiji cha Manyanyi kilichopo Kata ya Nyahongo. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu imekamilika mwaka 2010. Ujenzi wa bwawa la Kanyisambo haujaondolewa, bali haukufanyika kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kujenga mabwawa nchini, hususan katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kwa kipindi cha mwaka 2002/2003 hadi mwaka 2010/ 2011, Serikali imejenga na kukamilisha mabwawa saba ya Chereche, Irienyi 1, Irenyi 2, Ochuna, Nyanjagi, Barack Parish na Nyambori. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya

ujenzi wa mabwawa nchini kote likiwemo bwawa la Kanyisambo kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za muda mfupi za kupunguza tatizo la maji kwa wakazi wa Kata ya Nyahongo, Halmashauri ya Wilaya ya Rorya kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA),* imetekeleza miradi minne ya visima. Miradi hiyo imefungwa pampu za mkono katika Kijiji cha Nyamkonge.

**SPIKA:** Ahsante. Swali la nyongeza Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Licha ya kwamba Mkoa wa Mara tumezungukwa na vyanzo vingi vya maji, lakini wananchi wa Mkoa ule hasa akinamama tumeendelea kuteseka kwa kukosa maji.

Katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri anaainisha kwamba upembuzi yakinifu ulikamilika mwaka 2010 na anakwenda mbali kwa kusema kwamba watatekeleza kuchimba hilo bwawa la Kanyisambo wakishapata hela. Lakini mbaya zaidi anaainisha visima vinne ambavyo vimechimbwa kwenye Kijiji cha Nyamkonge bila kuzingatia umbali kijiografia kwa wakazi wa Kata ya Nyahongo.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini sasa Serikali itaipa kipaumbele Kata hii ya Nyahongo na kuchimba hilo bwawa la Kanyisambo ili kupunguza adha ya maji kwa wananchi wa hii Kata?

La pili, wananchi wa Tarime wamekuwa wakiendelea kupata adha kubwa ya maji. Kwa mfano, Tarafa ya Inchugu yenye Kata ya Susuni, Mwema, Sirari na Nyamaraga, tangu tumepata uhuru hatujawahi kuchimbiwa hata bwawa moja. Napenda kujua ni lini Serikali itawapa kipaumbele wananchi wa Tarime kama ilivyo kwingine Tanzania ili na sisi tuweze kupata hilo bwawa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na mimi kwamba Serikali imefanya mambo makubwa sana katika Mkoa wa Mara hasa katika Mikoa ya Ziwa Victoria kwa kuweka miradi mikubwa. Sasa hivi tuna miradi mikubwa ambayo inajengwa pale Musoma kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wa Musoma maji.

Mheshimiwa Spika, tunao mradi mkubwa utakaojengwa kutoka Misungwi kwenda Magu na Bariadi kwa kutumia chanzo cha Ziwa Victoria; tunao mradi mkubwa wa kupanua mtandao wa maji Ziwa Victoria kwenda katika maeneo ya Vijijini milimani kama Ilemela; na tunao mradi mkubwa wa kutoa majitaka katika Mji wa Bukoba. Kwa hiyo, Serikali imefanya mambo makubwa. Lakini tatizo hili ni kubwa, nimwahidi kwamba tutaendelea kuweka vipaumbele kulingana na fedha zinazopatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini katika Vijiji kumi ambavyo tumekuwa tukivitekeleza, mapendekezo yalianzia kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, pale itakapoonekana Kijiji hiki ndiyo muhimu zaidi, basi wao walete mapendekezo, Serikali itakuwa tayari kutoa ushirikiano.

**SPIKA:** Ahsante. Tunakwenda Wizara ya Elimu na Maendeleo ya Ufundi. Mheshimiwa Kaika Telele atauliza swali hilo.

Na. 108

**Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi *(VETA)* Nchini**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiahidi mara nyingi hapa Bungeni kuwa itajenga Vyuo vya Ufundi *(VETA)* katika Wilaya zote nchini:-

(a) Je, kwanini mradi huo umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu?

(b) Je, Wilaya ya Ngorongoro ipo katika awamu ya ngapi ya utekelezaji wa mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeahidi kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* katika WIlaya zote nchini kwa vile ni ahadi iliyotolewa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 na 2010. Katika kutekeleza azma hii, Serikali imedhamiria kujenga Vyuo vipya au kutumia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa ujenzi wa Chuo cha Wilaya ya Makete umeshakimilika na kinatarajia kuanza masomo mwezi Mei, 2013. Aidha, Serikali imeanza maandalizi ya awali ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya ya Ludewa, Namtumbo, Chunya, Kilindi na Ukerewe na katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, sambamba na jitihada hizo, Serikali itaviwezesha Vyuo 55 vya Maendeleo ya Wananchi vilivyoko katika Wilaya mbalimbali nchini ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi stadi. Kwa mwaka 2012/2013 Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi tayari vimejengewa uwezo na vimeshaanza kutoa mafunzo ya ufundi stadi ambapo kila kimoja kimedahili wanafunzi 50.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ngorongoro ni kati ya Wilaya 50 ambazo bado hazijafanyiwa utafiti wa kubaini stadi. Zoezi hili litafanyka mara fedha zitakapopatikana. Nachukua fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro kutumia Vyuo vya *VETA* vya Oljoro, Njiro na Chuo cha *St. Joseph (VTC)* kilichopo Loliondo Wilayani Ngorongoro kupata mafunzo ya

Ufundi Stadi wakati jitihada za Serikali za kujenga Chuo cha *VETA* katika Wilaya ya Ngorongoro zikiendelea.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Telele, swali la nyongeza.

**MHE. KAIKA S. TELELE**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

(a) Kwa kuwa azma hii ya Serikali ya awamu ya nne ya kujenga Vyuo vya *VETA* katika kila Wilaya hapa nchini, ni azma njema sana. Lakini basi ni kwa kiasi gani nia hii njema imezingatiwa katika bajeti ya mwaka huu?

(c) Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Wilaya ya Ngorongoro kutoka Arusha ni zaidi ya kilometa 400 na ina mazingira magumu kwa maana ya kwamba barabara hakuna. Sasa Serikali kutuelekeza tutumie Vyuo vya *VETA* vya Oljoro na Njiro ni kazi ambayo ni ngumu sana. Sasa Serikali inaweza kutuonea huruma na kutuingiza katika awamu ya kwanza ya kufikiriwa kupewa Chuo Kimoja angalau katika Jimbo la Ngorongoro?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa alitaka kujua tu bajeti ya mwaka huu wa fedha 2013 kwamba tumetenga kiasi gani kwa ajili ya Vyuo vya Ufundi vya Wilaya? Kwenye swali langu la msingi nimesema kwamba tunavyo Vyuo vinne ambavyo tayari maandalizi yake yanaendelea kutafuta hati miliki kwa ajili ya Halmashauri kukabidhi *VETA* ambayo ni Wilaya za Kilindi, Ukerewe, Namtumbo na Chunya na tulitenga Shilingi bilioni nne.

Kuhusu swali la pili ni kwamba kule Ngorongoro ni mbali sana na hivi Vyuo ambavyo nimevitaja vya Oljoro na kule Arusha, lakini nimesema kwamba stadi hizi za kazi zilifanyika kwa kuona kila Wilaya ambako hakukuwa na Chuo chochote hata kama ni cha binafsi au mashirika ya dini.

Wilaya ya Ngorongoro kipo Chuo cha St. Joseph *(VTC)* ambacho ni Chuo binafsi, ndiyo maana Serikali haikuweza kufanya stadi kwenye maeneo hayo. Lakini tulikuwa tunaangalia zile Wilaya ambazo hazina Vyuo kabisa.

**SPIKA:** Ahsante. Muda jamani tunakwenda nao. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

Na. 109

**Chama cha Walimu Kuwakopesha Walimu ili Kujikwamua Kimaisha**

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE** aliuliza:-

Walimu wamekuwa wakikatwa 2% ya mshahara kuchangia Chama cha Walimu Nchini, lakini wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu:-

Je, Chama hicho hakioni umuhimu wa kuwakopesha Walimu mikopo isiyo na riba kama ujenzi wa nyumba ili kuwakwamua katika mazingira magumu ya kimaisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makato ya asilimia mbili ya mishahara ya Walimu kama ilivyo kwa Vyama vingine vya Wafanyakazi nchini ni kutetea maslahi ya Wanachama wao.

Mheshimiwa Spika, shughuli hizo ni kudai nyongeza za mishahara, kupandishwa madaraja, kudai madeni mbalimbali kama malimbikizo ya mishahara, uhamisho, matibabu na nauli za likizo pamoja na kutetea Walimu wenye kesi mbalimbali kwenye Mahakama pale wanapopata matatizo wakiwa kazini.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Walimu Tanzania kinaona upo umuhimu wa kuwapokea Walimu kutokana na michango inayotokana na makato ya asilimia mbili ya mishahara yao. Kwa sasa Chama cha Walimu Tanzania kipo kwenye hatua za mwisho kabisa za kufungua Benki ya Walimu ambayo itaanza kufanya kazi mwezi Juni, 2013 na ikapoanza, kila mwalimu atakuwa na haki ya kukopa kwa ajili ya mahitaji yake kama vile kujenga nyumba, kusomesha watoto wake au kujisomesha yeye mwenyewe na mahitaji mengine.

Mheshimiwa Spika, suala la msingi ni kwamba mikopo itakayotolewa na Benki ya Walimu haiwezi kukosa kuwa na riba kwa vile chombo kitakachowakopesha kinatakiwa kuwa endelevu. Nafuu itakayotokana mikopo kutoka katika Benki hii ya Walimu ni kwamba riba itakuwa ya kiwango kidogo zaidi ikilinganishwa na Taasisi nyingine za fedha ambazo zipo kibiashara zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa, napenda tu niseme ukweli kwamba nasikitika na majibu haya ambayo hayaelezei hali halisi Mwalimu. Siyo kweli kwamba hii asilimia mbili inamsaidia Mwalimu kutatua matatizo yake. Kama ingekuwa hivyo, Walimu wasingekuwa wanagoma, Walimu wasingekuwa hawaingii madarasani kufundisha. Wangefanya kazi zao kwa ufanisi zaidi na watoto wetu wangefaulu vizuri.

Swali la kwanza, kwa sababu majibu yamekuwa yakitolewa humu ndani kwamba Walimu walikaa wakakubaliana hii asilimia mbili ikatwe na wakajaza fomu, jambo ambalo siyo kweli. Mimi pia ni Mwalimu na nimeshawahi kukatwa hizi asilimia bila makubaliano yoyote. Je, wapi walikaa wakakubaliana hiyo asilimia mbili? Kwanini iwe asilimia mbili na isiwe chini ya asilimia mbili? *(Makofi)*

Swali la pili: Je, Walimu wameshirikishwa kutokana na makato yao haya ya 2% ili kuweza kuanzisha hiyo Benki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira!

**WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, hii 2% ni kwa Vyama vyote vya Wafanyakazi na ipo kisheria kama nilivyogusia jana. Lakini ni kwamba kabla mfanyakazi hajakatwa hiyo pesa, Chama cha Walimu kinatakiwa kuwasiliana na Mwalimu kupitia Mwajiri sehemu ya kazi kuwaeleza na kuwaomba wajiunge na Chama hicho na kuwaomba wajaze fomu inayoitwa *TOF 6*.

Sasa kwa upande wa Walimu, Chama cha Walimu kinakwenda Halmashauri, kinawasiliana na Mkurugenzi. Kwa hiyo, *assume* kwamba Chama cha Walimu ndiyo Chama chenye Wafanyakazi wengi katika shule zote. Mkurugenzi anakubaliana na Chama cha Walimu waendelee kukatwa 2% lakini kwa wale ambao hawajaingia katika Chama, *assumption* ni kwamba kwa kuwa 50% ya Walimu wote wameshaingia katika Chama cha Walimu, wanakatwa hela inatwa pesa ya Uwakala.

Mheshimiwa Spika, hii pesa ya Uwakala ni kwa ajili ya kuwatetea wale Walimu ambao siyo Wanachama. Hata hivyo, maelekezo tuliyotoa ni kwamba Walimu wapya wanaojiunga na kazi wasikatwe hiyo pesa mpaka Chama cha Walimu kitoe elimu kiwaeleze na kiwapelekee hiyo fomu ili wajaze, na pia wajaze fomu ya kukubali makato. Hiyo tumeshawaelekeza Chama cha Walimu watuletee idadi ya Walimu waliojaza fomu ili tujue kuwa waliojaza fomu kweli ni 50% kusudi wengine wote waweze kukatwa hiyo 2%.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, naomba muwe mnaangalia na saa halafu tutakuwa tunaelewana vizuri. Mkiwa mnataka tuseme mpaka mwisho, haiwezekani. Muda wa Maswali umekwisha, sasa ni matangazo ya kazi.

Kwanza kabisa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii - Mheshimiwa Margareth Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa leo saa 7.00 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ambacho kitafanyika Ukumbi Namba 133, halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa - Mheshimiwa Rajab Mohammed anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 na kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo kwenye ukumbi wa Pius Msekwa C.

Halafu Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa Zakia Meghji, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tarehe 25 saa 7.15 watakuwa na kikao katika ukumbi namba 227. Halafu Katibu wa Wabunge wa CCM Bungeni anaomba niwataarifu Wabunge wa CCM kuwa leo saa 7.00 mchana kutakuwa na Kikao cha Wabunge wote wa CCM ukumbi wa Pius Msekwa.

## MWONGOZO WA SPIKA

**SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba!

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) inayohusu Mwongozo. Kwa ajili ya muda, naomba nisisome. Tangu jana mjadala wa bajeti ya Serikali ya Maji unaoendelea hapa unatoa ishara kabisa kwamba bajeti iliyoletwa na Serikali bado haijaendana sawasawa na hali halisi ya maji Vijijini na Mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Waziri Mkuu aliwahi kutamka kwamba katika ziara zake alizofanya alijionea hali halisi ya maji hapa nchini, na kwa kuwa leo katika maelezo yake ameona kuwa Serikali imeliona suala la maji na uzito wake na inatambua umuhimu wake, lakini ameelezea tatizo ni namna ya kuangalia mambo ya fedha na kuona wapi wanaweza kupata  kuweza kuziweka fedha.

Mheshimiwa Spika, tumekuja hapa kuwapa majibu Watanzania. Uliunda Kamati Ndogo ya Wabunge ambayo umeiita Kamati ya Bajeti, nami ni Mjumbe katika Kamati hiyo na ninaamini katika mijadala ambayo imekuwa ikiendelea, Kamati ile inaweza kuishauri Serikali vizuri na ikaisaidia nchi hii kuweza kupata fedha kwa ajili ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hata mjadala ukiendelea hapa itakuwa malalamiko tu siyo majibu, kwa nini usitoe mwongozo wa Serikali kukutana na Kamati ndogo ya Bajeti, *think tank* yako uliyoiweka pale ili iweze kurekebisha mahesabu na tukija hapa tuweze kuwapa Watanzania matumaini waweze kupata maji? Leo hii ukiwauliza Wanyiramba...

**SPIKA:** Mwongozo siyo hotuba jamani!

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, kwa nini usitoe muda kwa Serikali kukutana na Kamati hiyo?

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nami naomba Mwongozo wa Spika kwa Kanuni 68 (7).

Mheshimiwa Spika, wakati Naibu Waziri anajibu maswali yangu ya nyongeza mawili hususan swali nililouliza la Tarime ya Tarafa ya Inchugu kutokupata bwawa takribani miaka 52 baada ya uhuru, hakujibu kabisa, matokeo yake akaanza kuainisha miradi aliyoifanya ya Ilemela, Misungwi, Bukoba na kwingineko; nilikuwa naomba Mwongozo wako, likitokea jambo kama hili ambapo Mawaziri hawajibu maswali yetu, badala yake wanakuwa wanapiga siasa, ni hatua gani unachukua? Naomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Haya, ahsante. Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, niliomba Mwongozo jana kuhusiana na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha akijibu swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ufafanuzi huo alioutoa Mheshimiwa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Ndiyo!

**SPIKA:** Tulisema Mwongozo wa Spika siyo hotuba.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Kwa kifupi sana.

**SPIKA:** Naomba tuelewane vizuri, kwanza ningeomba ukae kwanza. *Aspect* ya Mwongozo siyo mahali pa kujadili, ni kitu ambacho wewe hufahamu kilichotokea kabla. Sasa namna ya kufanya; kwa mfano, hata jana mimi sikuwepo hapa, alikuwepo Mheshimiwa Naibu Spika, lile lako kuna maelezo binafsi, ile ya kwako ili-*fit* vile.

Hata alivyozungumza Mheshimiwa Lugola jana, pale ni maelezo binafsi ambayo yanakupa nafasi ya kujieleza vile. Lakini sasa Mwongozo unakuta ni hotuba, ni mabishano, Mwongozo hautaki namna hiyo. Someni kifungu cha Mwongozo.

Kwa hiyo, nawaombeni sana, hilo suala lako limekaa kama maelezo binafsi, na kifungu cha maelezo binafsi kipo. Tukitumia muda huu kusema Mwongozo kumbe tunahutubia, hatutakuwa tumelitendea haki Bunge. Nawaombeni sana, lile suala lako nimelisikia vizuri, haliwezi kuwa Mwongozo wa Spika. Ile ni maelezo binafsi, na wengine nao wakajiandae waje wajibu, lakini siyo kwamba tutaanza kubishana kama ilivyotokea. Kwa hiyo, lile suala la Mheshimiwa Mwigulu nitajibu baadaye, suala la Mheshimiwa Esther tutaangalia Maswali na Majibu kwasababu yote yako kwenye *Hansard*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 - Wizara ya Maji

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaite Wafuatao kama wapo kwasababu kusudio la Wizara hii tunataka tufike asubuhi tu, kama wapo Mheshimiwa Rita Mlaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Herbert Mtangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Mfaki, kama wapo naomba waanze halafu tutaendelea baadaye. Mheshimiwa Ritta Mlaki nilifikiri nimemwona!

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri na Wizara yake kwa hotuba nzuri pamoja na mapendekezo mazuri kwa ajili ya maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam ina watu takribani milioni 4.5 ambao wanakaribia kufika milioni tano wakati wowote. Jiji la Dar es Salaam limepata matatizo ya maji kwa muda mrefu na ninashukuru kwenye bajeti imejieleza kwa kirefu mikakati ya nyuma na mikakati ijayo.

Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 2002, Serikali ilitenga ama ilichukua mkopo wa Benki ya Dunia Shilingi bilioni 174 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji Mkoa wa Dar es Salaam ili upatikanaji uweze kuwa mzuri. Lakini ninasikitika kwamba pamoja na jitihada zote hizo, pamoja na kumweka Mkandarasi ambaye ilikuwa ni Kampuni ya Kichina, mpaka sasa bado Jiji la Dar es Salaam maji hayatoshi.

Pamoja na hayo, kuna matatizo mbalimbali yanayotokea katika Jiji letu kama milipuko ya magonjwa *Cholera* na magonjwa mengine ya kuambukiza ambayo

kusema ukweli yanaletwa kwa ajili ya uchafu hasa maji ambayo yanapatikana kwa shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi tumeona kwamba mabomba mengi katika Mkoa wa Dar es Salaam yamekatwa, watu wanaiba maji kwa kukata mambomba na kuteka maji, lakini vilevile wanapomaliza kufanya namna hiyo, hayaungwi kwa hiyo, kunakuwa na upotevu mkubwa sana wa maji kwa mpango huo.

Vilevile mambomba yaliyopo ni ya zamani ambayo yameziba na hayawezi kupisha maji kwa kiwango ambacho kinahitajika kwa sasa. Lita tunazotaka kutumia au zinazohitajika kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni lita milioni 470 kwa siku ambapo Waziri ameeleza kuwa mpaka sasa hivi tunapata lita 300 na kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya tatizo hili kubwa, tulikuwa tunapendekeza, Serikali sasa badala ya kuweka hizi *project* ndogo ndogo ambazo tunaona vyanzo vya maji kutoka Ruvu Chini, Ruvu Juu, Mtoni na visima ambavyo vinachimbwa hayatoshi, kwa nini Serikali isifikirie sasa kuweka *desalination plant* kubwa pale Dar es Salaam ili tuweze kutumia maji ya bahari?

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni kigugumizi kwa muda mrefu kutumia maji ya *Lake Victoria* lakini tunashukuru Serikali ikaamua na maeneo mengi sasa katika Kanda ya Ziwa yanapata maji na bado yataendelea kupata maji. Hebu tufikirie sasa mpango huu wa maji kutoka baharini.

Mheshimiwa Spika, tukiwaza namna hiyo watu ni rahisi kufikiria kuwa ni pesa nyingi na bajeti haitoshi au Serikali haina pesa. Lakini kuna mikopo. Nina hakika kuna nchi mbalimbali zitakuwa tayari au Benki ya Dunia hiyo hiyo kutukopesha kwa ajili ya *plant* kubwa kama hiyo ya kusafisha maji ya bahari tuweze kuyatumia kwa matumizi ya binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa sasa hivi ninashauri Serikali wafuatilie hayo mambomba kwa karibu mno. Kuna watu

wengi ambao wameajiriwa, kuna *DAWASCO*, kuna *DAWASA* ambao wanapita katika majumba kufuatilia bili zao, wanaweza vilevile kuamua sasa wakishirikiana na Manispaa husika kuhakikisha kwamba tunaweza kuziba hiyo mianya. Maji yanayopotea ni asilimia kubwa sana ambayo tunayaona na tuna uhakika nayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali sasa iwaze sasa kujenga *reserve tanks*. Nakumbuka katika mwaka wa 2004/ 2005 Serikali ilijenga *reserve tank* kubwa pale Kunduchi katika mwinuko katika kiwanda cha Wazo na hiyo ilitusaidia sana kupata maji katika maeneo ya Kata ya Kunduchi katika Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mbalimbali ambayo yako katika mwinuko kule Ubungo Chuo Kikuu ambayo tunaweza pia kujenga matanki makubwa ya maji yakasaidia kuwa kama *reserve* ili tuweze kuyakinga yale maji na kuyaweka tayari kwa kuweza kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea pia tatizo la majitaka katika Jiji la Dar es Salaam. Majitaka ni tatizo kubwa sana na imekuwa kama ni kitu cha kawaida, unapita eneo unakuta maji yametoka ya *sewage* yanamwagika barabarani na watoto wadogo wanachezea katika majumba ya watu.

Mheshimiwa Spika, sijui Serikali ina mpango gani katika hili. Ni kazi kubwa kwasababu miundombinu ya zamani iliyowekwa ya majitaka imezeeka kwa sasa na niseme njia ambayo ilikuwa imejengwa kwa ajili ya zile *sewage tanks* ambazo zilikuwa zimejengwa au njia ya kupeleka baharini nyingi zimeziba: Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia hili suala hasa katika Jiji ambalo lina watu takribani milioni tano?

Mheshimiwa Spika, eneo la Mikocheni B, ukipita pale ni harufu kali kuanzia kwa Nyerere mapa ufike njia Panda ya Kawe, inasikitisha sana. Maji yatoka mengi, yatoka viwandani, yanatoka kwenye vyoo, yanakuja kama bahari na kule

baharini sijui kumezibwa! Ningeliomba hilo Serikali itazame kwa makini sana, kwa sababu ni hatari kwa maisha ya binadamu, ni hatari kwa watoto wetu, ni hatari kwa viwanda na ni hatari pia kwa kila maendeleo yanayofanyika katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile watu hawa wa *DAWASA* wawe wakali kidogo kwa watu ambao wanachukua maji machafu na kuyaweka katika mitaro ya maji masafi.

Kwa hiyo, *drainage system* pale kwa ujumla haijakaa vizuri. Tunaliomba hilo liweze kufikiriwa. Tatizo la maji nchi nzima ni kubwa, tatizo la maji katika Miji Mheshimiwa Waziri amesema angalau 86% katika Miji wanapata maji. Lakini kwa Dar es Salaam nina hakika ni 55%.

Mheshimiwa Spika, nakumba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali yake watusaidie sana tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja nikiamini kabisa kuwa Mheshimiwa Waziri amesikia, Watendaji wake wamesikia, wawatusaidia katika mpango wa dharura tuweze kupata maji kwa haraka katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Herbert James Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Mfaki. Mheshimiwa Mntangi hayupo, Mheshimiwa Mfaki hayupo...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mfaki yupo!

**SPIKA:** Yupo!

**MBUNGE FULANI:** Eh!

**SPIKA:** Aah, Mama Mfaki; haya, ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa. Baada yake atafuatia Mheshimiwa Anna-Marystella, na Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia.

**SPIKA:** Naona kama husikiki vizuri.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuzungumza yale ambayo yanahusu Wizara hii, naomba uniruhusu niotoe shukrani.

Pamoja na kwamba umesema hapana, lakini mimi naomba niseme machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani za dhati kwako wewe binafsi, Naibu wako, Katibu wa Bunge, pamoja na wote ambao kwa kweli kutokana na hali yangu ya kuumwa mlinisaidia sana, mkaniwezesha nikatibiwa Muhimbili, nikaenda India na bahati nzuri nimerudi sasa hali yangu ni nzuri. Nawashukuruni sana. *(Makofi)*

Vilevile niwashukuru Madaktari wa Mkoa wa Dodoma akiwepo Mama Chaula pamoja na wenzake kwa msaada walionipa na kunitibu katika Hospitali yetu ya Dodoma na wakaruhusu niende Muhimbili.

Vilevile niwashukuru Madaktari wa Hospitali ya Chenai kule India wakiongozwa na Dkt. Rajah ambao kwa kweli walihangaika na mimi katika matibabu mpaka nikapata nafuu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumze machache kuhusu Wizara hii ya Maji, kwanza niishukuru Wizara ya Maji kwa Mkoa wetu wa Dodoma ikiwemo Mji wa Dodoma kwamba wamejitahidi sana kusambaza maji, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile niiombe Serikali, maji yamesambazwa lakini bado kuna tatizo la maji taka, maeneo mengi bado maji taka hayajatengenezewa miundombinu yake. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie sana juu ya suala hili, ni maeneo mengi ya Mji wa Dodoma hayana mtandao wa maji taka, kwa hiyo, hilo naomba lishughulikiwe.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ningeomba nishukuru sana kuhusu kuanza utafiti wa bwawa la Farkwa kule Kondoa. Naomba utafiti huo ufanyike haraka kwani lile bwawa likishakamilika litakuwa ni msaada sana kwa vijiji vilivyo jirani na kwa maeneo ambapo maji yatapita mpaka kufika Dodoma Mjini. Kwa hiyo, Serikali ijitahidi kufanya utafiti haraka na bwawa lianze kuchimbwa na likamilike mapema ili liweze kusaidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji kwa kweli ni la nchi nzima, imeonekana kwa kuwa kila Mbunge amejaribu kusemea suala hili, nisingependa niendelee kulisemea kwa sababu tayari limekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kazi ambayo ifanywe na Serikali ni kutafuta pesa. Fedha ikitafutwa naamini miradi hii ya maji vijijini inaweza kabisa ikapunguza tatizo la maji vijijini. Tunaomba hasa wangalie vijijini ambako wananchi wanapata shida sana hasa Mkoa wa Dodoma. Naamini ninyi nyote mnajua shida ya Mkoa wa Dodoma, ni Mkoa ambao hauna mvua za kutosha. Kwa hiyo, tatizo la maji ni kubwa na naamini pengine inawezekana ni kubwa hata kuliko mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutakapopata pesa, naomba sana Serikali ijitahidi kuondoa tatizo la Mkoa wa Dodoma, wakishachimbiwa mabwawa ya kuvunia maji, nina

uhakika mabwawa hayo yatasaidia sana. Pia kuchimba visima ambavyo vitasaidia kwa vijiji vingine.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ijitahidi kutafuta hizo hela na iweze kuendelea kutatua tatizo la maji Vijijini, kuchimba visima, kutengeneza mabwawa ili yaweze kusaidia.

Mheshimiwa Spika, sikuwa na mengi nilitaka kusemea hayo tu, kwa sababu mengi yameshasemwa sana na Wabunge na kwa kweli limeonekana ni tatizo kubwa kuliko kawaida.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa John Mnyika atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Nitaomba nizungumze mambo machache yanayohusiana na hotuba hii iliyopo mbele yetu ya Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Spika, naungana na Wabunge wenzangu wote waliokataa kuunga mkono hoja hii kuweza kupitishwa hapa Bungeni kutokana na kutokukidhi haja ya idadi ya fedha zilizopo katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, pia nieleze tu masikitiko yangu tarehe 4 Februari, 2013, niliwasilisha hoja binafsi hapa Bungeni juu ya hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa maji. Hoja ile iligusa maeneo makubwa mawili ambayo taarifa hii iliyotolewa na Wizara sasa hivi ya utekelezaji kwenye hotuba ya Waziri, bado sijaridhika kwamba imekidhi haja.

Mheshimiwa Spika, upande mmoja wa hoja ulihusu masuala yaliyohusiana na mpango wa maji Dar es Salaam, ambapo ndani ya kitabu hiki cha Waziri kuna mambo ambayo Waziri ameyatolea maelezo ambayo sijaridhika

nayo na ndiyo maana siungi mkono hoja na naungana na wote ambao hawaungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili wa hoja ulihusu masuala yanayohusiana na mradi wa maji vijijini ambao unatekelezwa Dar es Salaam lakini unatekelezwa vile vile kwenye Halmashauri zote za Wilaya nchi nzima. Tafsiri yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, kama wakati ule Serikali ingetakiwa kutoa majibu kwa ukamilifu kwa maazimio yote nane ambayo yalipaswa kutolewa majibu wakati ule, kuanzia mwezi Februari Serikali ingekuwa imeshaanza kuhangaika kutafuta pesa za nyongeza za kuongeza kwenye bajeti ya maji na kwa kweli tusingefikia katika hatua hii tuliyoifikia hivi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni rai yangu kwa Wizara, Serikali na kwa Wabunge wenzangu safari hii michango tuliyoitoa na michango tutakayoendelea kuitoa isiwe ya kinafiki ya kuonesha kukataa kuunga mkono hoja, lakini baadaye mkishakaa vikao vya Chama chenu mnaamua kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili ya muhimu sana hapa ambayo ni muhimu yakazingatiwa. Kwanza ni ukweli kwamba, kuna tatizo la uhaba wa pesa, lakini la pili ambalo ni kubwa zaidi kuna tatizo la matumizi mabaya ya pesa kwenye miradi ya maji na jambo hili ni muhimu Wizara kwenye majumuisho ikaja na majibu ni kwa nini kuna kigugumizi cha kumruhusu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kukagua pesa zilizotumika na ufanisi wa mradi wa maji ya mabomba ya Wachina ambayo hayatoi maji mpaka hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana tutaingiza pesa nyingine kwenye miradi, lakini kama hatushughulikii miradi ya zamani ambayo ni matatizo matupu, hizi nazo zitakwenda vibaya. Ni kwa nini kuna kigugumizi kila Mbunge anayesimama anasema Wakandarasi kwenye miradi ya Vijiji Kumi wengine

walichakachua ndiyo maana wametafuta maji na hayakupatikana. Ni kwa nini kuna kigugumizi kwa Serikali kumruhusu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za Mradi wa Vijiji Kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda sitakwenda kiundani, lakini ukaguzi wa kawaida tu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa taarifa iliyoishia mwezi tarehe 30 Juni, 2011 iliyowasilishwa Bungeni kuanzia ukurasa wa 99 wa ripoti ya *CAG* mpaka ukurasa wa 117 wa ripoti ya *CAG*, umeainisha namna ambavyo Halmashauri 98 za Tanzania zilivyoshindwa kutumia ipasavyo fedha za miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata tukienda kuongeza pesa kama hatuwezi kushughulikia ufisadi na ukiukwaji wa taratibu kwenye miradi ya maji, hatuwezi kufika kunakostahili. Kwa hiyo, hiki kielelezo nitaomba kifike mezani kwako ili Serikali ikubali kwenda kufanya ukaguzi kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, hapa nina Ilani mbili za Uchaguzi za CCM, nina Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 mpaka mwaka 2010 na nina Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015. Tukianza na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, CCM iliwaahidi Watanzania mwaka 2005 kwamba ifikiapo mwaka 2010 asilimia 65 ya wananchi vijijini watakuwa na maji safi na salama, ifikapo mwaka 2010 asilimia 90 ya wananchi Mijini ikiwemo Dar es Salaam watakuwa na maji safi na salama. Mwaka 2010 umefika ilani hiyo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama ilani hii haijatekelezwa ni kwa vipi na katika hili kabla ya mtoa hoja hajaja kutoa hoja, wachangiaji wengine wakishamaliza kuchangia, nitaomba unipe nafasi niweze kutoa hoja hapa ya kuahirisha huu mjadala kwani ahadi aliyoitoa leo Waziri Mkuu asubuhi ni ahadi ambayo ni maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, tukishapita kwenye kupitia vifungu kwa vifungu kwa mujibu wa Kanuni zetu, Bunge likikaa kama Kamati mchezo kimsingi utakuwa umemalizika. Tutaambiwa

hizo pesa zinatoka kwenye *OC*, zikitoka kwenye *OC,* sisi tumeshapitia vifungu kwa vifungu, ni wakati gani tutapitia tena kifungu kwa kifungu ili kuhakikisha kama kweli Wizara ya Maji tuliyoyasema yametekelezwa? Siamini kabisa hii ahadi ya Waziri Mkuu itatekelezwa kwa ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu tulipopiga kelele kuhusu bajeti ya Nishati na Madini mjadala ukaahirishwa, Waziri Mkuu aliahidi kwamba tunakwenda kukata kwenye *OC* tunatengeneza mpango wa dharura wa umeme. Ahadi ilipokuja hapa Bungeni hawakukata kwenye *OC,* wakasema wanakwenda kukopa benki kwa ajili ya mpango wa dharura wa umeme ambao mpaka sasa haujatekelezwa kwa ufanisi kwa sababu fedha hazikutolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa ni nini kinatufanya tuamini leo kwamba pesa zitakwenda kukatwa kwenye *OC* kama hatutapitia kifungu kwa kifungu mpaka tujihakikishie kwamba kweli pesa zipo.

Mheshimiwa Spika, nitaomba baadaye nitoe hiyo hoja ili tuahirishe mjadala kama Kamati inakaa na Serikali ikakae, tusiuziwe mbuzi kwenye gunia, tuletewe hapa, tukiziona pesa kifungu kwa kifungu zikienda kwenye miradi ya maji. Pia sikubaliani na Kamati kwamba tunahitaji bilioni 181 tu peke yake. Ukisoma hotuba ya Waziri kwenye hii *program* ya matokeo ya haraka *Big Result Now*, inasema pesa zinazohitajika kwenye maji ni trilioni 1.85.

Mheshimiwa Spika, trilioni 1.85 kama tunakwenda kwa kasi hii ya bilioni 181, tutahitaji miaka mingapi ili kutatua tatizo la maji hapa nchini? Kwa maneno mengine, kinachohitajika hapa ni kama tulivyofanya mpango wa dharura wa umeme. Katika mpango wa dharura wa umeme tulisema tunatafuta bilioni mia tano, hapa tukitumia bilioni mia tano; mwaka wa kwanza bilioni mia tano, mwaka wa pili bilioni mia tano, mwaka wa tatu bilioni mia tano, tumemaliza tatizo la maji nchi nzima siyo Dar es Salaam tu.

Mheshimiwa Spika, hii inawezekana, bilioni mia tano ni nusu tu ya mapato ya Serikali kwa mwezi, tukiamua kujifunga mkanda kwa mwezi mmoja tu tunapata pesa ya kwenda kuinusuru nchi na tatizo la maji.

Mheshimiwa Spika, kuna Mbunge alichangia jana akasema maji ni uchaguzi, lakini naona maji ni zaidi ya uchaguzi kwa sababu maji ni maisha ya watu! Kama ninyi mnashindwa mnatazama uchaguzi peke yake 2015 ondokeni madarakani watu wengine waingie watekeleze haya. Maji ni maisha ya watu na maji ni maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja na siungi mkono maelezo yaliyotolewa na Waziri Mkuu asubuhi kwa sababu sina imani na ile kauli mpaka tupitie kifungu kwa kifungu, tuzikate hizo pesa kwenye *OC* tuzione, tuzielekeze kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuna nyongeza kidogo Dar es Salaam na ni jambo zuri, kuna mkopo wa India umeongeza pesa Ruvu Juu, kuna mkopo wa Marekani umeongeza pesa Ruvu Chini kwa maana ya pesa za *MCC*.

Mheshimiwa Spika, lakini ni vizuri Waziri akakumbuka, mwezi Februari walipokaa kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri na Rais akaja akafanya mkutano na Waandishi wa Habari akatangaza tatizo la maji Dar es Salaam litakuwa historia mwaka 2013. Huu ni mwaka wa 2013, pesa zilizotengwa wakati ule zilikuwa ni bilioni 654, kwa hiyo hizi zilizotengwa hapa pamoja na kuwa zinaonekana ni nyingi ni chini ya mpango wa Serikali, ni chini ya ahadi ya Serikali na kama hatutazingatia haya...

**MBUNGE FULANI:** Dakika kumi hazijafika kweli?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, wale wananchi wa Dar es Salaam wako tayari kuendelea kuandamana kuja Wizarani kwako, kwa sababu wamekwishachoka. Waliahidiwa tatizo la maji itakuwa historia mwaka 2010, halijawa historia. Wakaahidiwa mwaka

2011, halijawa historia, mwaka 2012, halijawa historia na mwaka 2013, halijawa historia!

Mheshimiwa Spika, katika hili hakuna masuala ya Vyama, Itikadi, sijui na nini. Maji ni maisha, maji ni uhai na maji ni utajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya sijui yupo? Kama hayupo atafuata Mheshimiwa Mary Chatanda, kama hayupo atafuatia Mheshimiwa Jerome Bwanausi, naye pia hayupo. Mheshimiwa Josephine Chagula, wamekwenda wapi hawa? Mheshimiwa Sylvester Koka, hayupo; Mheshimiwa Fatma Mikidadi, naye hayupo; Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Chiligati na Mheshimiwa Rosemary Kamili na Mheshimiwa Joshua Nassari wajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Mengi yamesemwa na mengi yatasemwa, lakini tukubaliane kimsingi kwamba kinachotakiwa ni upatikanaji wa pesa.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nipo kwenye Kamati ya Bajeti na kila Mbunge anayesimama hapa analia kilio cha maji, nadhani katika hili hata ndugu zetu wa upande wa Upinzani wataunga mkono hoja ili pesa ipatikane twende kutatua kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia ukurasa wa 52 na hili ninalisema kwa makusudi wakati ndugu yangu Mheshimiwa Machali anachangia alisema kwamb,a kuna sehemu zinapendelewa na mradi ule unaongelea suala la Miji inayozunguka Lake Tanganyika. Katika Miji inayozunguka Lake Tanganyika Kasulu siyo mmojawapo, lakini wamepata pesa za kutosha na nyingi tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri tunapokuwa tunatoa kauli tuwe tunakumbuka na yale tunayoyasema. Tanzania hii ni ya kwetu sote, tusiigawane nchi kwa vipande vipande, naiomba Serikali ihakikishe kwamba tatizo la maji ni kwa Tanzania nzima, kwa hiyo tuiangalie Tanzania kama nchi yetu sisi sote, pale ambapo mradi unakuwa umekwenda sehemu moja tusiwe watu wa kulaumu, ni zamu imefika kwa mwenzako itakuja zamu yako itafika, tuwe na *spirit* hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashangaa kuna baadhi ya wachangiaji walikuwa wanasema eti Mheshimiwa Maghembe mradi umekwenda Same na Mwanga kwa sababu yeye ndiyo Waziri kipindi hiki. Hizi ni fikra potofu sana, kwa nchi hii si vizuri tukawa tunakwenda kwa mtazamo huo, ule mradi ulikuwepo kabla hata yeye hajakwenda kwenye sekta hiyo. Kwa hiyo, haiwezekani eti kwa sababu leo wananchi wa Same na Mwanga wanapata maji na Korogwe ndiyo iwe nongwa, hii siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu la Kalambo na Wilaya mpya ya Kalambo, ukitazama miradi ni michache sana. Naamini ndiyo maana safari hii tumesema kwamba mpaka dakika ya mwisho tutaifumua bajeti na baada ya kusikiliza maoni ya Wabunge walio wengi basi kilio kitasikilizwa na kutekelezwa yale ambayo yanatakiwa. Naamini na Wilaya ya Kalambo na Vijiji vyake, mwambao wa Ziwa Tanganyika kuanzia Kipwa kule tunakopakana na Zambia, nasi tutasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana mwaka huu kuna wanafunzi wawili walikamatwa na mamba wakiwa wanatafuta maji na wale ndiyo wako Ziwa Tanganyika, lakini maji safari hii yanakwenda Kasulu sisemi sana, lakini ujumbe umefika.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Kipwa, unakwenda Kilewani, unakwenda Kasanga Port unakuja Muzi na vijiji vyote vile vya Ziwa Tanganyika, hali ya maji ni ya tabu kweli. Ndiyo maana kila mara inapofika kipindi cha masika magonjwa

ya kuhara na kipindupindu ni kila mwaka. Naamini Wizara inasikia, ihakikishe kwamba, huu mradi wa kwenda kuleta maendeleo na kuleta maji unafanyika kwa nguvu kubwa.

Mheshimiwa Spika, siyo vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika peke yake ambavyo vina shida ya maji ni Kijiji kama Kalepula, Ulumi ambapo Waziri alifanya ziara na aliahidi yeye mwenyewe, naamini wakati anahitimisha atawaambia wananchi wa Kijiji cha Ulumi ni lini maji yatakwenda. Pia atawaambia wananchi wa Kafukula ni lini maji yatakwenda na wananchi wa maeneo mengine. Ninachowaomba ndugu zangu tushikamane katika hili, maji ni kwa Watanzania wote, hivyo hata Wizara zingine hawatapata tabu pale watakapoambiwa kwamba *OC* imepungua ili twende kutatua kero ya maji.

Mheshimiwa Spika, naamini hata ikifika kwa Vyama vya Upinzani wakiambiwa kwamba ruzuku inapungua ili tukatibu kero ya maji hawatasikitika na katika hilo hata wao naona wanapiga makofi. Tukubaliane kimsingi kwamba maji ni tatizo, hivyo ni lazima sisi zote tufunge mikanda tuhakikishe kwamba tunawapelekea Watanzania maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwanzo ilikuwa nisiunge hoja, lakini kutounga mkono hoja maana yake ni nini? Maana yake unasusa na sisi hatujafundishwa tabia ya kususa, unapambana unahakikisha kwamba, unatatua tatizo. Kwa hiyo, naamini Serikali, itakuja na majibu mazuri sana kwenda kutatua kero ya maji. Kwa sababu nataka kuhakikisha kwamba, kwamba, *we are promise solvers,* twende tukatatue kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono baada ya majibu mazuri ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Kamili atafuatiwa na Mheshimiwa Joshua. Mheshimiwa Rose Kamili dakika tano na Mheshimiwa Joshua Nassari dakika tano.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa pia. Napenda kuchangia Hotuba ya Waziri, lakini naomba nianze na kusema siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo, sio kwamba, hatupendi maji yaende Mwanga, wala Same, wala Korogwe, lakini utaratibu uliotumika sio sahihi kwa sababu, Watanzania wote tunalia maji. Watu wanatembea kilomita 20, akinamama na wazee wote na vijana wanatafuta maji, lakini leo bilioni 56 ziende kwa awamu moja kwa mwaka mmoja Mwanga, sisi hatukubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hizo fedha tuzigawanye, ziweze kwenda Hanang, kwa ninyi msiotaka acheni, sisi Hanang tuna shida ya maji. Tunahitaji bilioni 19 ambazo ni fedha zilizotolewa na *OPEC, USD* milioni 12 zije kwetu kwa sababu, katika bajeti yake Mheshimiwa Waziri alisema, *estimate* iliyofanyika ni bilioni 32 tu ndio zianze kazi, mradi wa mwanzo wa mwaka huu; sasa wewe mwaka huu hela zote unapeleka kwako, kwa nini tusione wivu? Hatukubaliani nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, sio kwamba wao wana shida ya maji sana, Mwanga Mjini wana maji, vyanzo vya maji vipo, mnakwenda kuchimba kule Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo linakauka kiangazi saa nyingine, kwa nini usiende kwenye Milima ya Kindoroko au Lambo? Maji yakateremka kwa *gravity* badala ya kutumia fedha nyingi? Hapa hamkutumia utaratibu mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumza kwamba, Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wizara, wana dharau kwa Wabunge. Hatujapitisha hii bajeti, Hotuba yake jana ndio alisoma. Gazeti la jana limetangaza tenda ya Mwanga, hivi kweli Waheshimiwa Wabunge, hatujadharauliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gazeti la Mwananchi liko hapa, tangazo la Mwanga tayari kwa ajili ya tenda ya kujenga au kuanza mradi. Nani amempitishia hiyo hela na nani

alimwambia atangaze kabla hatujapitisha? Hiyo anatudharau sisi, tunataka hizo hela tuzigawanye, tangazo lake akalifute ili tuweze kufanya kazi inayotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la visima kumi; fedha zimekaa kwenye akaunti gani? Ameeleza kwenye Hotuba yake yeye mwenyewe kwamba, fedha zimepatikana 2012 zilikuwepo; 2013 ndio zinatolewa Machi, zilikuwa kwenye akaunti ya nani na zilikuwa zinafanya nini? Akatukwamishia miradi yetu ya maji ya visima vitano ambavyo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika Hotuba yake ya Bajeti ya 2012/2013, alitamka hapa na kwenye *Hansard* ipo, alisema kwamba, visima vitano-vitano kwenye kila Kijiji, mradi wa visima kumi utakamilika; haujakamilika mpaka leo, anatwambia nini sasa sisi Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu unasema visima vitano tena. Wilaya ya Hanang, iko hapa kwenye kitabu chako, umeonesha kwamba, ni visima viwili; inakuwaje visima viwili na vingine vitatu viko wapi? Nataka kuvijua kwa sababu, tunapopitisha maana yake tayari kuna wengine watakosa vile visima vitatu wasipate hayo maji.

Mheshimiwa Spika, wana Hanang wana shida sana, Watanzania wana shida sana, lakini kwenye mradi wa visima 10 umekuwa ni fedha za kuliwa kuanzia ngazi ya Wizara nadhani au kama sijui ni Hazina, sijui, lakini kule Halmashauri nako ni sawa na ile Katuni inayoonesha kwamba, unamega hapa, unamega tena, yule bata akifika kwenye Halmashauri wanamalizia na ile meza yake kabisa, ndio kitu kilichofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niambiwe pia, zile fedha milioni 700 mlizopeleka zimefanya nini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naona muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nassari, dakika tano!

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa sababu, ya muda, leo naomba niende moja kwa moja kuzungumzia mambo ya wananchi wangu wa Arumeru Mashariki, waliyonituma hapa.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Mbunge, bila kuhonga shilingi, sikuwahi kumnunulia mtu kanga wala kumnunulia mtu sukari. Wananchi wa Arumeru Mashariki, waliniamini kwamba, naweza kuja kuwasemea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kangi Lugola, jana ametoa nyoka wa shaba hapa. Nikim-*complement* yule nyoka wa shaba ambaye alikuwa amechorwa, leo nakuletea picha zilizopigwa Jimboni kwangu Arumeru Mashariki, takribani wiki moja iliyopita kuonesha ni jinsi gani ambavyo wananchi wanahangaika na adha ya maji.

Mheshimiwa Spika, nilishawahi kuzungumza hapa, nikasema maji sio kama umeme; unapokosa maji hata ukipewa soda, huwezi kuishi. Ukikosa umeme unaweza kuwasha kibatari, unaweza ukatumia *petrol* ukawasha jenereta, mambo yanakwenda. Lakini ni aibu leo miaka 52 ya uhuru wa nchi hii, bado tunajadili tatizo la maji kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu kubwa sana unakwenda kwenye Jimbo kama Arumeru, ambalo lina Mlima Meru wenye maji mazuri ambayo hayajawahi kukatika hata siku moja. Jimbo lenye Ziwa kama Ziwa Duluti ambalo lina maji ya kutosha ambayo hayajawahi kukatika hata siku moja. Jimbo lenye Ziwa Momela ambalo lina maji; Jimbo lenye vyanzo vya maji kama vya *Ngaresero Lodge,* vya Tema kule Nkwaranga na maeneo mengine, lakini cha ajabu wananchi hawana maji ya kunywa ilhali wako kilomita moja kutoka umbali wa chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, ni aibu sana, katika picha hizi ninazokuonesha hapa leo na kwa sababu na wewe ni mama,

naomba zifikishwe mezani kwako uzione. Kuna mama hapa, ambaye ni mama kama wewe, ambaye yuko na punda ametembea kilomita saba kwenda kufuata maji, anatoka katika Kijiji cha Samaria kwenda Kikatiti kutafuta maji kilometa saba. Hapa hapa kuna picha ya watoto tarehe 20 Aprili, juzi, siku ya shule saa 5.00 asubuhi wako wanatembea kutafuta maji, maana yake wanakosa shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii nitamshangaa Mbunge yeyote, ambaye ataunga mkono bajeti hii. Wananchi wanatuona vizuri kwa sababu, wanatuona kwenye *TV,* Mbunge yeyote anayeunga mkono bajeti hii, wananchi Watanzania mnatusikiliza, hafai kurudi kwenye Bunge hili mwaka 2015. Tunajadili maji miaka 52 ya uhuru, halafu kuna Mbunge anasema Watanzania tuna maji 80%; 80% ya wenye maji vijijini ni akina nani hao? Yuko nchi gani huyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajadili maji hapa, halafu anakuja Waziri anatudanganya. Jana kwenye Hotuba yake hapa, wazi kabisa tena uwongo mkubwa, Waziri analidanganya Bunge? Ameandika kitabu hiki hapa anasema kuna Kijiji kinaitwa Kasanumba, ambacho kwa mwaka huu ambao unakwisha keshokutwa mwezi wa Sita, wameshatekeleza mradi wa maji wa Vijiji Kumi wakati hata Kasanumba, hakijawahi kuwepo kwenye nchi hii; amekitoa wapi? Amekitoa Mwanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa tuambiwe vizuri hapa. Pia tunaambiwa kwamba, kuna Vijiji vitano ambavyo vimetekelezwa, Kasanumba ambacho hakipo, Kikuletwa, Mbuguni, Kwa Ubora, Namboreni, Mwaivaro; wakati leo ukienda Arumeru ni Vijiji viwili peke yake ambavyo visima vimechimbwa, tena yakafukiwa na yakafungwa, hayajawahi kutoka, hayajawahi kunywewa wala hayajawahi kufanyiwa chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakwenda wapi? Kama Wabunge, tunadanganywa hapa halafu tunashangilia,

kidumu Chama cha Mapinduzi – kidumu Chama. Kidumu namna gani kwa hali hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa niseme wazi, Mheshimiwa Mnyika amesema hapa kwamba, atatoa Hoja ya kuomba kuahirisha Mjadala; naomba kila Mbunge aunge mkono, Serikali, ikakae chini ijichimbie, ituletee majibu sahihi ya maji hapa. Mbona akina Magufuli wanaweza kwenye barabara, anashindwa vipi kwenye maji? Anashindwa vipi? Profesa na Dokta, wako wawili wasomi, wanashindwa vipi? Naomba tusaidiane katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini aibu nyingine watu wanakufa. Jimboni kwangu Arumeru kuna wananchi wamekufa, kuna yatima wameachwa kwa sababu, wazazi wanahangaika kutafuta maji mpaka usiku wa manane kwa baiskeli, wanagongwa na magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Kata yangu ya King'ori, kuna mama ameacha watoto ndani kwenda kutafuta maji usiku, nyumba ikawaka moto, watoto wawili wakaungua, wakafa wote; naambiwa niunge mkono, nitaunga vipi mkono bajeti hii? Haifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa unyenyekevu mkubwa na niwaombe Wabunge wenzangu wa Chama cha Mapinduzi, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wao ndio wanaunga mkono hoja baada ya malalamiko marefu kwamba, tukubaliane leo tuahirishe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, muda wako umekwisha.

Mheshimiwa Chiligati atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale na Mheshimiwa Christine Ishengoma ajiandae.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nichangie katika mjadala huu wa maji. Kwanza nikubaliane na wenzangu waliotangulia kusema kuhusu tatizo kubwa la maji na ni kweli kwamba, katika kero za wananchi hapa Tanzania, sasa hivi inayoongoza ni kero ya maji. Tatizo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hapa tunataka kujadili jinsi gani ya kukabiliana na hii kero yenyewe. Tusipoteze muda mwingi sana kushutumiana, kulaumiana, kunyosheana vidole, wananchi wanataka waone jinsi gani sisi nyumba hii tunaisaidia Serikali, kutatua tatizo hili, hilo ndio jambo kubwa ambalo liko mbele yako. Wala siungi mkono hoja kwamba, baadaye tuahirishe kuzungumza, tuzungumze sasa hivi mpaka tumalize, kwa nini tuahirishe jambo ambalo linawakabili wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hoja nyingi zimetolewa zenye lengo la kutufikisha kwenye kutatua tatizo lenyewe na wananchi ndio wanasubiri. Moja ambalo limetoka hapa ni kwamba, bajeti ni finyu haitoshi na kwamba, sasa tutafute namna ya kuiongeza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri Mkuu, asubuhi. Wakati anajibu maswali, nadhani lilikuwa ni swali la Mheshimiwa Mbowe, ametoa ahadi kwamba, watakaa kutazama, wanyofoe katika mafungu ya *OC* mbalimbali, ili bajeti ya maji iongezwe. Nadhani hili, kwa muda mfupi tuliunge mkono, wala tusitie mashaka. Kuna rafiki yangu mmoja kasema yeye ana mashaka kwamba, hii kauli ya Waziri Mkuu ina mashaka; kwa nini tuwe na mashaka na Waziri Mkuu?

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu hawezi akasimama hapa, akatoa kauli ambayo hataitekeleza. Kwa hiyo, naiomba Serikali, itekeleze ule ushauri wa asubuhi wa Waziri Mkuu, watazame baadhi ya mafungu yale ya *OC,* tunyofoe nyofoe ili tuongeze bajeti ya maji, tutatue tatizo la maji ambalo wananchi wa Tanzania wanasubiri majawabu ndani ya nyumba hii. Wananchi hawasubiri malalamiko, wanasubiri

majawabu, kwa hiyo, moja ya majawabu tupunguze katika mafungu mengine ya *OC,* tuongeze bajeti ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni la muda mfupi, lakini kwa muda mrefu tunaishauri Serikali, kwamba, tatizo hili tusiendelee kulitatua kwa utaratibu wa kawaida, kwa bajeti ya kawaida, *business as usual,* hatuwezi. Lazima tutafute hata mbinu zingine zaidi ya huo utaratibu wa kawaida. Wala huu mradi wa *World Bank,* tusiutegemee sana kwa sababu, kwa miaka mingi haujaonesha matunda, twende zaidi nje ya *box.*

Mheshimiwa Spika, watu wameshauri hapa na nakubaliana nao kwamba, hebu sasa tuunde chombo kingine, kama kwenye barabara tumeunda chombo (*TANROAD)* na kinafanya vizuri, barabara tunaziona.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye umeme tumeunda chombo (*REA),* kinafanya kazi nzuri na matunda tunayaona. Hebu nayo maji haya nayo tuyaundie chombo ambacho kitapata bajeti ya Serikali, kitapata mikopo ya nje na ndani, ili tuongeze bajeti ya maji.

Mheshimiwa Spika, hii inawezekana kabisa, tuwe na kitu kama *REA* kwenye umeme na kitu kama *TANROAD* kwenye barabara, hivyo kwenye maji nako tunahitaji chombo kama hiki. Nadhani Serikali, hili mlichukue na mwakani tutakapokuja tusije katika hali kama hii, tuje katika hali nyingine yenye kuleta matumaini makubwa zaidi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende Manyoni. Wilaya ya Manyoni, kuna sehemu mbili, moja iko juu kwenye *plateau,* moja ni Bonde la Ufa. Sasa kwenye bonde la ufa ndio tuna shida kubwa kabisa ya maji. Ni shida kubwa kwa sababu, tukichimba kule kwenye bonde la ufa, ama hupati maji au unapata maji ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaishauri Serikali na Mheshimiwa Waziri nimeshamweleza tatizo hili kwamba,

tusiendelee kuchimba kule kwenye bonde la ufa kwa sababu, ama tunakosa maji ama tunapata maji ya chumvi; mkitaka kutusaidia, tumewaambia.

Mheshimiwa Spika, pale kwenye Salanda *escapment*, ule mwinuko wa Salanda pale, wamechimba visima, maji ni mengi. Naishauri Serikali kwa mara nyingine, hebu chukueni maji kwenye mwinuko wa Salanda kule, kuna eneo linaitwa Mbwasa, visima tayari vipo na vina maji mengi. Yale maji sasa myateremshe kwenye vijiji vyote vya bonde la ufa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nilishamkaribisha aje atazame eneo hilo, alishanikubalia na nadhani Bunge hili kabla halijakwisha tutakwenda nimwoneshe. Tukifanya hivyo Mheshimiwa Waziri, lile bonde la ufa, Wilaya ya Manyoni, ambalo lina shida kubwa kabisa ya maji hiyo shida itakwisha kwa sababu, maji yapo tena unayateremsha kwa *gravity* kwa sababu, *Salanda escapement,* mwinuko ule uko juu na vijiji vyote viko chini ya bonde huku. Ni kutandika mabomba na kuweka matenki, maji yanakwenda tu kwa kumiminika kwa sababu ni *gravity*. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, kabla Bunge halijakwisha twende nikamwoneshe hilo eneo; alishanikubalia, bajeti yake ikishakiwisha namkaribisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabla kengele haijalia, suala la uvunaji wa maji. Hili nalo Serikali tumeishauri, lakini tumelifanyia mzaha mzaha mwingi sana, sasa tuache. ngazi mbili, ya kwanza, kila mtu anayejenga nyumba ya bati au ya vigae kuwe kuna Kasheria kakumlazimisha achimbe lile tenki la chini pale, maji yakitoka kwenye bati lake yaende chini, ni akiba yake. Hili linawezekana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ngazi ya Serikali, mito hii ya muda, wakati wa msimu mito inapitisha maji mengi sana, lakini kuyakinga inabidi tupate mabwawa madogo madogo, nalo ni jambo ambalo hatujaliwekea mkakati. Naishauri Serikali, tuweke mkakati, kila Mto tuuzibe tu, tutapata maji ya kutosha kabisa. Hata sisi ambao tuko katika maeneo ya ukame huwa

tuna mvua fupi, maji yanapita yanapotea. Sasa maji yale tunataka kwanza tuweke mkakati wa Wizara na Halmashauri zetu, tuweze kuziba ile mito, tupate mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanjale atafuatiwa na Mheshimiwa Ishengoma na Mheshimiwa Juma Nkamia ajiandae.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya maji. Kwa kweli, tatizo la maji ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika tathmini ya haraka haraka kwa kweli, maswali mengi yanayoulizwa hapa yanahusu maji. Hiyo inaonesha kwamba kweli, tatizo la maji ni kubwa na hakuna Mbunge hapa ambaye atasema ana usalama katika Jimbo lake kuhusu ya maji.

Mheshimiwa Spika, maji ni tatizo kubwa na nafikiri tutashutumiana hapa, tutatukanana, tutasema haya na yale, lakini hayatasaidia kitu kwa sababu, hata tungemwambia Maghembe, hela atapata wapi? Si ni lazima sisi tuamue hapa, tuzungumze hapa kitu cha maana hela zipatikane kuhakikisha kwamba, tunamsaidia Mheshimiwa Maghembe na mwenzake, wapange mipango vizuri tena, lakini suala la maji ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, tunahitaji kwamba, suala hili lingekuwa ni tatizo la ku-*solve* kwa haraka kwa sababu, kuna miradi ya maji ya Vijiji Kumi imekwenda zaidi ya miaka 10, hata kijiji kimoja kinashindwa kutekelezwa. Kwa hiyo, nina maana kwamba, kwa hela ya Benki ya Dunia, kwa kweli, hapa tumeshindwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni vizuri Serikali, iangalie mfumo mpya wa kutafuta hela zingine, vyanzo vingine vya fedha, lakini kwa Benki ya Dunia, hapo nasema kwamba, kwa kweli, tumeshindwa. Kama kuna miradi imetekelezwa kwa hela ya Benki ya Dunia ni michache sana.

Mheshimiwa Spika, miaka 10 vijiji 10 havijakwisha. Tutakwenda miaka zaidi ya 30 hapa kumaliza Vijiji Kumi na mfano, mimi nina vijiji 148. Kwa hiyo, katika vijiji 148 ina maana mpaka watu wote tutakuwa tumeshakufa humu ndani ndio watapata maji wengine, kwa hiyo, kuna faida gani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ni vizuri vyanzo vingine vya fedha za maji vitafutwe na ingekuwa ni vizuri hela hilo zipatikane sasa, kwa mwaka huu 2013/2014. Tukienda 2014/2015, wananchi wataona hapa sisi tunakwenda kwa ajili ya uchaguzi tu, wala haitakuwa na tija. Naomba itafutwe hela ya kutekeleza Vijiji hivyo Kumi viishe wakati huu 2013 na 2014, angalau tuanze kwa hapo, maana vijiji ni vingi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba, kwa kweli, suala hili la maji limetusikitisha sana kwamba, halitekelezwi. Miaka yote tumejaribu kuzungumza, kila tukikaa hapa, ahadi ni zile zile, lakini maji hayaendi, tutafika wapi ndugu zangu?

Mheshimiwa Spika, mimi kwa pale Mbalizi, mji wangu ule wa Mbalizi, ni mji ambao una watu wengi wanaelekea kwenye 60,000 au 70,000. Nimeahidi maji muda mrefu kwamba, maji haya yataboreshwa, lakini mpaka sasa hivi inaelekea kwamba, katika bajeti, ukisoma vitabu hakuna kitu kinaoneshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali, ijitahidi kuhakikisha kwamba, miradi hii ambayo iko kwenye mpango,

kwenye programu, iishe kabla hatujafika huko mbele. Tuwe na historia na sisi kwa sababu, kama hawatapata maji kwa wakati huu, mwaka huu 2013/2014 kwa kweli, Mbeya itakuwa ni tabu; tunajiletea moto mbaya kabisa ambao utatuunguza.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali, iwe makini na nafikiri ni vizuri, kama walivyosema wengine, zitafutwe hela za haraka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, miradi hii ambayo kwa kweli ipo inatekelezwa kwa haraka zaidi. Nje ya hapo tutakuwa tunapiga kelele tu ambayo haitakuwa na maana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, itakuwa si vizuri kuzungumza jambo hilo hilo watu wote hilo hilo. Kwanza ingekuwa tangu asubuhi kuna hela mahali tungesema jamani, hata mjadala uishe, kama Serikali ingesema jamani kuna pesa zimepatikana mahali, tusingekuwa na maneno ya kusema hapa. Lakini watu wanapiga kelele, watu wanataka kulia humu ndani, wanazungumza kwa *emotion* kwa sababu, shida ni kubwa katika Majimbo yao; barabara angalau kidogo wanajitahidi, lakini suala la maji ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa maji ni kama hawapo, wako wachache sana, kwa hiyo, hata miradi ile ikiambiwa kwamba itatekelezwa, inachukua muda mrefu mno.

Mheshimiwa Spika, halafu pia pesa kutoka, ziende kwenye mradi huko nazo zinachukua muda mrefu mno. Kuna nini huko, Serikalini jamani? Tupatieni hela haraka, kama kuna mradi unatakiwa utekelezwe haraka, hela zitolewe kwa haraka lakini hela zinatolewa kwa shida kubwa sana. Kama hela hakuna si tuwaambie! Wananchi tumeshawaahidi tumewaambia vijiji hivi vitapata maji, wanasubiri miaka mitatu, minne, maji hayapatikani, tutaeleweka kwa watu? Unaweza kwenda kesho kifua mbele unasema jamani mnichague tena? Itakuwa ni mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iliangalie suala hili kwa umakini tena wa hali ya juu kabisa kuhakikisha kwa kweli maji yanapatikana kabla hatujafika mwaka 2014 zaidi ya hapo hakuna. Aidha, nawaomba ndugu zangu Wabunge, tuhakikishe kwamba Serikali kwa vyovyote vile, hata kama ungesema unanikata hela yangu, mimi ningesema sawa tu, cha msingi ni kwamba wananchi wangu wapate maji. Mtu mmoja hapa alisema jana 15% ya hela za *OC* ziende kwenye maji, tunasita nini hapo kama hatuna hela! Tukisubiri hela ya Benki ya Dunia hawa Wazungu wanatuchezea tu, wewe miaka kumi hela hazitoki, vijiji vimeshaainishwa tayari lakini hela haitoki na masharti yao ni makubwa mno. Kwa hiyo, tukiangalia na kufikiria hela za Benki ya Dunia, tutakuwa tumepotoka vibaya sana. Ni afadhali tufikirie hela zetu wenyewe, ombaomba mara nyingi anapata shida na mtu anayeomba mara nyingi kuna shida yake, kheri kutoa kuliko kupokea. Tunapokea kila siku, tunapokea mara nyingine kwa matusi na kwa shida na kwa dharau kubwa sana halafu mambo hayatekelezwi.

Mheshimiwa Spika, kule kwangu kulikuwa na mradi ambao ulishakubaliwa kuwa utapewa hela yake lakini umesumbua kwelikweli, mradi wa Iwahanje japokuwa sasa hivi wanatengeneza lakini umechukua muda mrefu. Hii inatokana na wataalam na hela ya benki wanasema masharti fulani mmekiuka, sasa hii ya masharti tutafika nayo wapi? Ndugu zangu wa Serikali, tunaomba hiyo hela ya maji vijiji kumi ipatikane kwa mwaka huu, tukienda mpaka mwaka kesho, mwaka 2014/2015 tumeshapotoka tayari. Watu watajua hawa ni waongo kwa sababu kwa miaka

kumi wametuvumilia na bado maji hawapati, mwisho watasema hawa watu waongo wameona uchaguzi ndiyo wanaleta maji wakati huu, naomba hela zipatikane mwaka huu. Mimi naomba hela zipatikane sasa na tuzungumzie hiyo Wabunge wenzangu, hela za vijiji kumi zipatikane sasa, siyo mwaka kesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya! Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, watu wote tunafahamu kuwa tatizo la maji ni kubwa sana hapa nchini na hasa vijijini. Maji ni changamoto kweli. Maji safi na salama bado ni changamoto kweli kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hali ya utoaji wa huduma ya maji hapa nchini mpaka sasa hivi ni 58.6% kwa wastani katika maeneo ya vijijini na wastani wa 86% katika maeneo ya mjini. Lengo letu tu nafahamu kuwa kuja kufikia mwaka 2015 ni 95% kwa mjini na 65% vijijini. Nashauri hii Serikali yangu tuweze kujipanga tutatue kero hii ya Watanzania hasa huko vijijini na hasa kina mama ambao wanateseka kila siku kutafuta maji. Kwa kusimamia na kutekeleza malengo na mipango yote, tunaweza tukafaulu kupatikana maji kwa hawa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni bajeti. Kama walivyosema Wabunge wenzangu, kila mmoja anasema kuwa bajeti imepungua na kweli bajeti imepungua kila mwaka. Kwa hiyo, naungana na wenzangu tuweze kuona ni wapi ambapo tunaweza kutafuta hela kusudi tuweze kuongezea bajeti na kutatua hili tatizo la maji hasa kwa Watanzania. Nashauri kuwa tuongee, tuangalie, ni wapi hasa tunaweza tukapata hela tukaweza kutatua hili tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa mazingira unachangia sana kutopata haya maji na nashauri wananchi na mipango mizuri ya Serikali ya kupanda miti. Kila mmoja anajua kuwa miti inasaidia kwenye kuleta mvua kwa pamoja tuweze kusaidia kulinda vyanzo vya maji na hasa kwa kupanda miti rafiki ya maji pamoja na kupanda mipaka kuzunguka vyanzo vya maji kusudi zisiweze kuharibiwa kwa sababu vyanzo vya maji vinaharibiwa na binadamu hasa kwa upande wa kulima na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni upande wa uvunaji maji. Uvunaji maji kwa makabila mengine ni tabia. Anapojenga nyumba ya bati, anaweka makinga maji. Kwa hiyo, naomba wananchi tuwe na tabia ya kuweka makinga maji angalau tuweze kuvuna maji ya kutumia nyumbani pia tuweze kuchimba mabwawa kwa matumizi ya mwaka mzima hasa wakati wa mvua wakati ambapo maji yanakuwepo tuyatumie tusiache yaweze kuharibika bure. Kwa hiyo, tuwe na mipango kabambe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwa Mkoa wa Morogoro napo bado hatujapata maji ya kutosha. Mara kwa mara tumeona Manispaa hata vijijini watu wamekuwa wanasumbuka sana kutafuta maji. Kwa hiyo, nashauri Serikali yangu, narudia tena tuweze kutafuta hela za kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Morogoro ni 64.5% vijijini ndio wanaopata maji na 62.3% mijini wanapata maji. Mtashangaa kwa nini mijini wanapata maji kidogo. Wanapata maji kidogo kwenye Manispaa kwa sababu Morogoro inapanuka, Manispaa inapanuka, kwa hiyo watu wamekuwa wengi wanahitaji maji, kwa hiyo, mipango kabambe iweze kuwekwa. Nashauri kuwa kwa kutatua hili tatizo, hii mipango mizuri ya vijiji kumi iweze kutimilika, ikitimilika tatizo la maji linaweza likapungua hasa kwa wananchi wote kwenye Halmashauri zote kwa sababu vijiji kumi vinapelekwa kwenye Halmashauri zote za nchi yetu ya Tanzania na Watanzania wanaweza kupata maji salama na maji safi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ujenzi wa Bwawa la Kidunda ni mpango mzuri sana. Bwawa hili linapatikana Mkoani Morogoro Vijijini na maji haya yatakwenda kuongeza maji kwenye Mto Ruvu ambayo haya maji yatasaidia kwenye Mikoa ya Dar es Salaam pamoja na Pwani. Ombi langu ni kuwa hivi vijiji vinavyozunguka hili bwawa na vyenyewe viweze kupata hayo maji, wananchi waweze kufaidi hayo maji pamoja umeme ambao utatokana na bwawa hili. Vijiji vyenyewe ni kama Selembala pamoja na Mzia, wananchi wana matatizo sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nilikuwa naomba tuweze kufikiria vijiji vya Mtego wa Simba, Lukole, Fulwe, Mikese pamoja na Mikumi, wana matatizo sana ya maji na wenyewe kwenye mipango hii ya maji waweze kupatiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongelea pia bwawa la Iguruba pale Isimani Iringa, ilikuwa ni gumzo sana lakini safari hii nimeona kama tumetengewa hela. Naomba hizi hela zote zilizotengewa ziweze kufika huko kwa wananchi kusudi waweze kufaidika kutumia hayo maji kwa kilimo pamoja na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana ila tatizo la maji bado ni kubwa, naomba tuliangalie kwa macho yote mawili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa ni Mheshimiwa Juma Nkamia, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar na baadaye.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu pia kwa kuniamsha salama ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, nisipoongelea tatizo la maji katika Wilaya ya Chemba, nadhani hukumu yangu itakuwa imebakiza miaka miwili na nusu tu. Nianze tu na hili suala la mradi wa Ntomoko, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja aliahidi na kwenye bajeti nimeona, naamini kwamba utafanikiwa na wananchi wa Kinkima kule, Churuku, Hamai na maeneo mengine watakuwa wanasubiri kwa hamu sana. Kina Mzee Ikanda kule wamechoka kila siku kutembea kwenda kufunga yale mabomba ili maji yatoke, naamini sasa suala hili litafikia kikomo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni suala la bwawa la Farkwa. *Project* hii imekuwa ikizungumzwa na katika bajeti ya mwaka jana ilitengewa shilingi milioni 800 tuliona wataalam fulani sijui ni wataalam au Wazungu walikuwa wanakuja kule, inawezekana ndiyo wanafanya jambo hilo. Kwa hiyo, tunaamini kwamba kama jambo hili litafanyika kwa haraka tatizo la maji katika Wilaya Chemba litakuwa limepungua. Naiomba Wizara ifahamu kwamba hili bwawa la Farkwa pia litumike kwa ajili ya kupeleka maji Chemba na si kuleta Dodoma mjini peke yake.

Mheshimiwa Spika, kwenye miradi hii ya maji ya *World Bank,* visima vya Benki ya Dunia, visima viko tayari vimechimbwa muda mrefu sana na vingine ambavyo vilikuwepo kwenye *project* ya benki ya Dunia nilivichimba mimi kwa kutafuta wafadhili, kinachotakiwa sasa ni kwa Wizara kupeleka hela tu kwa ajili ya kuweka *pump* watu wanywe maji. Jambo hili linachukua muda mrefu sana. Msera kuna kisima kipo tayari, Mwaikisabe kipo tayari, Chemba kipo tayari tena cha ajabu Chemba ndio Makao Makuu ya Wilaya hii ya Chemba hata kwenye bajeti ya mwaka huu hakipo wala hakihitaji zaidi ya shilingi milioni 55. Jenjeluse kipo tayari na kina maji mengi zaidi ya 80,000 *cubic per hour.* Nadhani vitu hivi ni vizuri tuangalie, Kelemakuu shimo lipo maji yapo tatizo ni hilo na Wizara waliomba tuwapelekee tumewapelekea, Chandama tuna matatizo, Mapango hali kadhalika na Jangalo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anisaidie jambo moja dogo sana, Mlongia tumechimba kisima sisi kwa fedha tulizotafuta wenyewe, kinatoa karibu lita elfu nane na kitu kwa siku kwa saa. Tukaambiwa tupeleke Wizarani ili waweze kukiingiza kwenye bajeti kwa ajili ya kufunga mitambo. Kila ukimuuliza Mhandisi anasema kwamba Wahandisi wa Wizara wamesema hawawezi kufanya lazima wao wenyewe waende Kondoa na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ikawaambia tuko tayari kuwagharamia kutoka Dar es Salaam mpaka Kondoa, miezi minne sasa jambo hili halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri jambo hili alitilie maanani, tatizo ni nini? Wahandisi wa Halmashauri hawaaminiki ama kuna nini hapa mpaka wataalam watoke Dar es Salaam waka-*verify* kwamba je kweli kisima hiki kipo? Basi naomba hawa Wahandisi ambao pengine hawawaamini Wahandisi wa Kondoa waende basi wakatusaidie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kisima cha Mlongia kinaweza ku-*save not less than twenty five thousand people* kikasaidia Jangalo kikasaidia Itolwa lakini tatizo ni suala la kufanya maamuzi tu. Najua kuna matatizo ya fedha, tofauti kwenye barabara, hela nyingi inakuwa *injected* kwenye barabara lakini maji ni muhimu sana hata ukipita juu ya barabara ya lami unahitaji kuoga pia. Kwa hiyo, naomba sana hilo mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna baadhi ya maeneo katika visima hivi ambavyo tulishachimba kwa mfano Ombili pale, tumechimba kisima kinatoa karibu lita 7,000. Nikaweka mashine mimi mwenyewe siyo chini ya shilingi milioni 25, *efficiency* yake ni kubwa zaidi kuliko hata zile mashine zinazowekwa na Halmashauri ama na Wizara. Kwa hiyo, ningeomba pengine wataalam wa maji wa Wizara watakapokwenda kama watakwenda huko Kondoa angalau wapite pale Ombili wafanye *feasibility study* kidogo, ni namna gani tumeweza kufanikiwa kufunga mashine pale Ombili kwa gharama ndogo sana ya shilingi milioni 25 na kisima kinahudumia bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema Waziri achote kidogo zile za kwenda Mwanga anipelekee pale Mlongia lakini Waswahili wanasema paka si rangi, umuhimu ni kukamata panya. Kwa hiyo, nakuomba jambo hili unisaidie.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nasema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja hii lakini kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kunipa afya na kuweza kusimama hapa leo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji, ni tatizo kubwa sana na Wabunge wote wamechangia. Yaliyowagusa katika Majimbo yao hata mimi ni hivyo hivyo lakini kuna msemo Waswahili wanasema ukitaka kumlaza mtoto mwimbie wimbo mzuri. Pia mtoto huyo ukimwimbia wimbo huohuo siku ya kwanza, siku ya pili, siku ya tatu inawezekana asilale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusema hivyo kwa sababu Jimbo langu la Nyang'wale leo ni mwaka wangu wa tatu nazungumzia suala hili la maji, matatizo ni makubwa sana katika Jimbo hilo. Ukiangalia matatizo hayo yamesababisha mpaka vifo kwa ajili ya kutafuta maji. Leo takribani mwezi wa pili kuna kifo ambacho kimetokea, kina mama wamegombana kisimani kwa ajili ya kugombea maji na mmoja ikawa amefikia kupatwa na umauti.

Mheshimiwa Spika, kwanza nasema siungi mkono hoja. Kwa nini ninasema hivyo, wananchi wa Jimbo la Nyang'wale kutokana na matatizo ya maji waliyonayo kwa muda mrefu watanishangaa sana kwa nini naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Serikali naiomba iongeze bajeti yake, bajeti hii haitoshi. Nikiangalia kwenye kitabu hiki tumepangiwa kama shilingi milioni 316, mimi nina kata 12 vijiji 54 na mahitaji ni makubwa sana kuliko hizo

shilingi milioni 316. Mwaka jana niliuliza swali hili la maji, nikaambiwa nimetengewa shilingi milioni 30 kwa ajili ya upembuzi yakinifu lakini pesa hizo hazijaingia na wala hazijulikani ziko wapi lakini maji haya yako ndani ya Jimbo langu, Ziwa la Victoria liko Jimboni kwangu, ni nusu kilomita tu lakini kijiji cha mwanzo kutoka Ziwani pale kinaitwa Nyamtukuza hakina maji na Jimbo langu kutoka Ziwa Victoria kwenda kijiji cha mwisho kwenye Jimbo langu ni kilomita 40 lakini Jimbo hilo halina maji. Niliishauri Serikali kwamba itenge pesa kwa ajili ya kufufua mtambo wa maji uliopo Ziwa Victoria pale ambao umesimama tangu mwaka 1975 na ulikuwa unasambaza maji zaidi ya vijiji 15 lakini hakuna jibu lolote mpaka leo hii, kwa hiyo, sina haja ya kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyosababishwa na maji, kuna matatizo mengi, maradhi mengi, minyoo, *typhoid* na malazi mengine ambayo yanasababishwa na unywaji wa maji machafu na yasiyo salama. Pia maji yamesababisha mimba zisizo rasmi kwa mabinti zetu, yamesababisha ndoa nyingi kuvunjika, yamesababisha hata wanafunzi wetu kutofanya vizuri katika mitihani yao kwa sababu ya muda mwingi kupoteza kwenda kutafuta maji. Kwa kweli Jimbo la Nyang'wale lina matatizo makubwa sana ya maji na maji yametuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa ushauri kwa Serikali yangu kwamba iwahamasishe sasa wananchi waweze kuchimba ama kujenga visima katika maeneo yao na pia katika shule za msingi na sekondari ili kuweza kupunguza tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu kuna maporomoko mengi ya maji, kuna mabwawa ambayo yameshapasuka zaidi ya miaka 15 na mabwawa hayo yalikuwa yanaweza kusaidia zaidi ya vijiji 15. Kuna bwawa la maji lililoko Nyang'hwale ambalo limebomoka zaidi ya miaka 15 na kuna bwawa ambalo limebomoka kwenye kata ya Shabaka, sehemu ya Shabaka panaitwa Nyamgogwa, bwawa lile na lenyewe lilikuwa linasaidia sana zaidi ya vijiji kumi. Kwa hiyo, naiomba Serikali, bajeti hii iongezwe ili na

Nyang'hwale iweze kupata maji na kupunguza tatizo la maji kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, mimi siungi mkono hoja mpaka Serikali ituongezee pesa katika bajeti hii ndiyo nitakapoweza kuunga mkono hoja kwa sababu wananchi wa Jimbo la Nyang'hwale hivi sasa wananisikiliza, tatizo ni kubwa sana. Viongozi mbalimbali wamefika katika Jimbo hilo, kina mama wanawaimbia vizuri, wanawakuta wamependeza ni kwa ajili ya ugeni huo lakini baada ya hapo ukienda ghafla kwenda kuwatembelea utakuta hali zao si nzuri kutokana na ukosefu wa maji. Viongozi wahurumieni hao kina mama ambao sasa hivi wanaota vipara kwa ajili ya kufuata maji kwa umbali mrefu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kina mama hao, wanawaimbieni kwa furaha, hawahitaji zile pesa ambazo huwa mnawatunza shilingi 2000/3000, wanahitaji muwahudumie hususani upande wa maji. Serikali ninaiomba ituangalie kwa jicho la huruma. Hata Mheshimiwa Rais alipokuja kwenye kampeni mwaka 2010, alituahidi kupata maji kutoka Ziwa Victoria. Mtandao huo siyo kwamba haupo, upo! Mpaka leo matenki ni mazima, baadhi ya mabomba yapo, tunashangaa kwa nini mtambo huo haufufuliwi na ni asilimia labda sabini na tano tu ulioharibika lakini asilimia ishirini na tano mitambo yote ni mizuri.

Mheheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alipotuahidi tulikuwa na matumaini mazuri. Mimi nasema kipaumbele cha kwanza kwa Jimbo la Nyang'hwale maji, kipaumbele cha pili maji, kipaumbele cha tatu maji, hatuhitaji umeme, hatuhitaji barabara, tunahitaji kwanza maji. Maji, halafu vifuate vitu vingine kama barabara pamoja na umeme, vyote ni muhimu lakini maji ni uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo siungi mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, halafu Mheshimiwa Abdulsalaam Ameir, yupo? Atafuatiwa na Mheshimiwa John P. Lwanji.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuungana na Mheshimiwa Moshi Chang'a, DC wa Wilaya ya Kalambo ambaye amefiwa na mke wake. Naomba Mwenyezi Mungu awape faraja na mazishi yatakuwa kesho saa tisa, kwa hiyo, naungana nao na Mungu awepe faraja.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwa huzuni kubwa juu ya tatizo la maji nchini Tanzania. Hali kadhalika nami siwezi kuwa kinyume juu ya suala hilo kwa sababu ni ukweli ambao uko wazi na wananchi wengi wanahitaji maji.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ambayo sisi Wabunge au viongozi tunaweza tukayaona kama ndiyo *priority* hasa kutegemea na taswira au dira ya nchi tunakotaka twende lakini ukienda kwa wananchi hawa wa kawaida, wao wana vipaumbele vyao na ni vile ambavyo vinawagusa katika maisha ya kila siku. Ukienda kuongea na wananchi, ukawauliza nini kipaumbele chao, wanaume watakuambia elimu, watakuambia barabara; wanawake watakuambia maji, watakuambia suala la afya. Hayo ndiyo mambo yaliyopo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, maji ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya kiuchumi. Kwa sababu kama hakuna maji salama, ina maana ndipo inakuwa chimbuko la magonjwa na ndipo tunapofikiria kuwa na dawa nyingi katika vijiji, dawa nyingi kwa ajili ya watu ambayo nayo yana athari katika miili yao. Kwa hiyo, kama tutaweza kuwa na maji safi na salama, tunaweza kupunguza bajeti katika maeneo mengine hasa ya afya.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vijijini hata katika Zahanati, unakuta hakuna maji safi na salama na ndiko wanakojifungulia akina mama, ndiko wanakopata magonjwa na ndiko tunapojaribu kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Maji yana mchango mkubwa katika kupunguza vifo vya akina mama na watoto hasa walioko chini ya miaka mitano, wasiojitambua na wanaoweza kunywa maji ambayo hayajachemshwa.

Mheshimiwa Spika, suala langu hili naomba nilielekeze katika sura hii. Wote tumezungumza juu ya tatizo hili, lakini tunalizungumza sasa. Najaribu kuona kwa upande wetu sisi wenyewe, kama Wabunge, hivi leo sisi Wabunge tukiulizwa katika mijadala yetu yote tunayoijadili humu ndani, kipaumbele chetu namba moja ni kipi, namba mbili ni kipi, namba tatu ni kipi? Mtakubaliana na mimi kwamba mara nyingi kadri ya bajeti inavyokuja hapa, kila bajeti inachangiwa kwa kipaumbele kilekile. Tukifungua sasa hivi *Hansard*, siku ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tukifungua siku ya Utumishi, tukifungua siku ya Kilimo, utakuta kila aliyechangia alitoa *priority* kwa eneo lile. Kwa hiyo, tunakuwa hatuna mawazo ya pamoja kwamba sisi tuko katika msimamo upi kama nchi.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba, kwanza pamoja na kwamba Mheshimiwa Spika unasema pongezi siyo za muhimu, mwanamke mwenzetu lazima tukupongeze kwa kutoa huu mtindo mpya wa kusema kwamba Bunge tuanze kujadili bajeti muda huu kabla ya muda ule ambao unatakiwa mwezi wa saba ili kuwezesha mabadiliko ya msingi. Suala hilo, watu wanaweza wakaliona ni mabadiliko madogo. Haya ni mabadiliko makubwa sana, yana *impact* kubwa sana na yana mchango mkubwa sana katika bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo basi, mimi najaribu pia kujiuliza. Kwa mfano, sasa hivi tunasema tukate kwenye *OC* sioni taabu lakini kila wakati napenda kujiridhisha. Hiyo *OC* tunayoikata ilikaa hapo kwa ajili gani? Nini maana ya *OC*, ipo hapo kwa ajili gani? Kwa sababu hata katika hii

miradi ya maendeleo, utakuta kama gari litahitajika kutumia mafuta kwenda kutembelea huo mradi au shughuli yoyote inayoendana na mafuta, *package* yake inajitokeza kwenye *OC*. Kwa hiyo, unaweza ukaweka pesa ya maendeleo ya kufanya ile shughuli ukajikuta hauna fedha ya kufuatilia ule mradi, nalo hilo ni tatizo. Pia, nasema kwamba tusiangalie *OC* kama kitu hasi, lakini tuende ndani zaidi. *OC* hii iliyowekwa hapa ni kwa ajili ya nini? Ile ambayo ipo kwa ajili ya mambo ya viburudisho, mambo ambayo siyo ya lazima, posho labda pengine kama za sisi Wabunge hapa ndani, basi hizo tunaweza tukasema labda pengine tupunguze sisi hayo lakini tuwezeshe ile miradi kuweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, katika hii miradi ya maendeleo huwa ina utaratibu wake wa mchakato. Kwa mfano, mradi huu uzungumziwa zaidi, mradi wa Same - Mwanga. Mradi huu haujanza leo na mpaka wale wanaotoa pesa wamekuja kuukagua wakaridhika, wakasema basi tutoe pesa kwa ajili ya mradi fulani ambao gharama yake ni kiasi fulani. Leo tukisema tunakata zile pesa tunapeleka sehemu nyingine, siyo hiari ya wahisani. Wahisani wetu wanapotoa pesa wanatoa kadri wanapovyojisikia na matakwa yao. Ndiyo maana unakuta kwamba, hata kama una shida kwenye eneo jingine, lakini kama wao kwa wakati huo siyo *priority* yao, unakuta hatuwezi kuhamisha. Kwa mfano, wao sasa hivi wao *priority* yao ni kusaidia vyama vya siasa, labda *priority* yao ni kusaidia demeokrasia, kwa hiyo, unakuta hata kama wewe unalia maji, kama hiyo siyo *priority* yao sasa hivi, hawawezi kupeleka pesa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nashauri mradi huo tusiupige, siyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Maji anatoka huko, basi wananchi wake wapate shida, eti kwa sababu sisi tunasema amepeleka kwao, hapana. Lazima wananchi wale watendewe haki sawa na wananchi wa maeneo mengine. Mradi huu mimi kwa kumbukumbu zangu naamini ulipita wakati wa Waziri wa Fedha, tena Mheshimiwa Mkulo hapa amenipa ushahidi na wengine siku za wa nyuma hata wakati huyu Waziri hajawa kwenye eneo hili. Tusimfanyie hivyo, wananchi sasa watasema tusimchague

mtu ambaye atachaguliwa kuwa Waziri kwa sababu tutakuwa tunanyimwa miradi, nadhani siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami kwa kusisitiza hilo, ukiangalia tatizo la maji katika Bonde la Ziwa Nyasa, maeneo ya Ngumbo, Nkili, Lundo, kwa kweli ni kubwa mno. Kuna visima vimechimbwa kule miaka nenda rudi mpaka leo havijaunganishwa. Hali kadhalika nikirudi upande wa Rukwa, bonde la Ziwa Rukwa, lile limekuwa *mapped* kama maeneo *chronic* kwa magonjwa sugu ya kuhara. Kila mwaka Mkoa wa Rukwa lazima upate aibu ya kipindupindu katika bonde la Ziwa Rukwa, *simply* kwa sababu maji yanatoka kule juu milimani yanaenda kule chini, hakuna visima, hakuna mabomba sawa na ambavyo Mheshimiwa Mbunge wa Singida, Mheshimiwa Chiligati alipokuwa anaeleza. Maeneo haya yanakaribiana sana tabia zake na za kule Singida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa mazingira kama hayo, mimi nachokiomba sisi kama Wabunge tukae pamoja lakini pia tushauriane na Serikali yetu, kuweza kuona hata sasa hivi kama tunaongeza hiyo hela inaenda wapi? Maana siyo tu kwamba tunapata *OC* shilingi milioni 600 tupeleke kwenye maji, lakini kwa mradi upi? Lazima ijulikane zinaenda kwenye mradi fulani na Fulani *otherwise* unatawanya hela na miradi haikamiliki.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni juu ya makandarasi wa maji. Makandarasi wa maji hawatutendei haki, wanalipwa hela hawatokei *site* kwa wakati....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa John Lwanji atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ali Salum na Mheshimiwa Lusinde ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, muda huu tunafikia mwisho wa mvua kwa msimu huu. Ni kipindi cha kipupwe sasa kinaanza lakini siyo muda mrefu watu wetu wataanza kuhangaika kutafuta maji. Kwa muda wa miezi saba inayokuja, kwa kweli ni kipindi cha kuhuzunisha na ni chakusikitisha.

Mheshimiwa Spika, nchi hii imepata misaada sana katika eneo hili. Wafadhili wengi wamemwaga pesa kwa ajili ya kutanzua tatizo la maji lakini tatizo hili linakuwa sugu. Kama alivyosema Mheshimiwa Chiligati, Wilaya ya Manyoni ina maeneo mawili, eneo la juu na la chini. Sasa mimi nakotoka ni kwenye *plateau*, lakini kila wanapochimba maji, maji hayapatikani, ni maeneno machache na pale yanapopatikana labda wataalamu huwa wamekwenda kushirikisha wenyeji wa maeneo hayo, wanaweza wakajua maeneo hayo maji yanaweza yakapatikana wapi, lakini mara nyingi magari yamekuwa yakija, yanaweka mitambo yao hapo, wanasimika mitambo na kuchimba maji lakini hakuna maji. Magari yamekuwa yakirudi na watu kuwaacha wakifadhaika. Wakati magari yanapofika watu wanakuwa na matumaini makubwa lakini magari yanapoondoka yanaacha huzuni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninashangaa sana jinsi tunavyopoteza pesa kwenye eneo hili. Katika mchakato huo, kuna watu wawili hapa, yule anayekwenda kutafiti maji, kujua eneo lile lina maji au hapana, ni mtumishi wa Serikali. Wanakwenda wanapima, wanasema eneo hili lina maji, wanaweka alama pale, halafu ndiyo mchakato wa tenda unaanza kumpata Mkandarasi wa kuja kuchimba lakini kwa bahati mbaya mara nyingi inatokea, anapokuja kuchimba huyo mchimbaji naye ni mtu mwingine; ndiyo kapewa tenda hiyo, sijui ni mtu binafsi anachimba pale na anatoka pale maji hakuna. Pesa iliyoteketea pale kwa kisima kimoja siyo chini ya shilingi milioni 30 na kuendelea, sasa hasara hii

imekuwa ikitokea kila siku, nani hasa anayeibeba, inamwangukia mwananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba tuwe *serious* kwenye eneo hili. Naomba huyo mtu basi atakayekuja kupima, basi apewe na dhamana ya kuchimba huyohuyo kwamba akipima pale akasema hapa kuna maji, basi huyohuyo yeye mwenyewe apewe kazi hiyo ya kuchimba kwa makubaliano kwamba kama maji yatapatikana utalipwa, kama hayakupatikana hasara ni juu yako wewe. Mimi nafikiri wangekuwa na uangalifu zaidi katika kutafiti na kupima maji, akisema hapa kuna maji, basi maji yawepo lakini utaratibu wa sasa hivi unaliingizia Taifa hasara na wananchi wanapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara hii iniambie basi juu ya ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mwaka jana alipokuja Mji Mdogo wa Itigi. Mhandisi wa Maji wa Wilaya alisimamishwa pale nusu saa, awaeleze wananchi juu ya mkakati unaofanyika ili kuupatia Mji Mdogo wa Itigi maji ya kutosha na mji huo unaandaliwa na baadaye utakapokuwa Wilaya ikute miundombinu ya maji ikiwa safi lakini nimeangalia kwenye kitabu cha bajeti sioni. Napenda kupata jibu, inaangukia wapi ahadi hii ya Rais ili watu waweze kuelewa kwamba kuna tofauti kati ya ahadi ya Rais na mipango ya kawaida. Mkuu wa nchi amekuja pale na akaahidi, baada ya Mhandisi kueleza, akasema nataka hii m-*fast truck,* akasema anataka kuona mji huu unapatiwa maji ya kutosha lakini sijaona mpango huu na mimi nasimama hapa Itigi siyo mbali, napigiwa simu, wenyeji wanakuja hapa mara kwa mara na leo ninao wageni hapa, wameniuliza je mpango wa Itigi kuhusu maji ahadi ya Rais aliyoitoa je, iko katika bajeti safari hii? Kwa hiyo, ninaomba majibu wakati wa kuhitimisha ili tuweze kutendeana haki.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, watu wa Rungwa walikuwa na bwawa miaka nenda rudi lakini kwa bahati mbaya sana, lile bwawa lilipopasuka, Serikali ilikuja na ahadi nzuri na ikatenga fedha wakati ule wa Bunge la Tisa, mwanzo tu tulipoingia hapa, ilitenga shilingi milioni 250, kujaribu kujenga kuta za bwawa hilo. Nasikitika mpaka leo

na mimi sioni *coordination* yoyote kati ya Wizara ya Maji na Wizara hizi nyingine zinazochangia kwenye miradi ya maji. Hii miradi ya *DADPS* sijui hii miradi inayochangiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na wao ile *coordination* yao iko *half hazard*, sijaona *seriousness* yoyote. Sasa wanachi hawaeliwi, wanachotaka ni maji. Hawahitaji kitu kingine. Naomba maelezo kuhusu hilo bwawa ili na mimi niweze kuona kama naunga mkono hoja au siungi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara hii ifanye utafiti juu ya maeneo ya Jimbo langu. Kata ya Idodyandole, Kata ya Gondi, Kata ya Sanjaranda, Kata ya Ipande, Kata ya Itigi, Kata ya Kitaraka mpaka kule juu unapoelekea Kata ya Mgando, Mitundu mpaka Mwamaghembe ni eno la juu, maji hayakai. Mvua zinanyesha vizuri lakini maji hayakai lakini kuchimba maji kama nilivyosema mwanzo linakuwa tatizo. Maji yanakuwa ni kirefu na mara nyingi maji hayapatikani. Ningeomba Serikali ifanye utafiti na ije na mkakati wa kuchimba mabwawa katika maeneo hayo. Ukiweka bwawa moja pale Idodyandole, ukaweka bwawa moja pale Kashanga, ukaweka bwawa lingine pale Mbungani, Kata ile utakuwa umeshamaliza. Kwa kweli, haya mambo mengine ya watu kutafuta maji waachwe, wafanye wao wenyewe, lakini maji ya uhakika kwa ajili ya wakulima na wafugaji wa maeneo hayo, yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi. Naomba sana tuwe *serious* katika eneo hili. Mimi sishangai kwa nini sasa hivi watu tunagombana hapa. Toka mwaka 1961 tatizo hili la maji mpaka hivi sasa bado limekuwa sugu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa mimi kama wenzangu wanavyosema katika kuliangalia tatizo hili, mimi naona eneo hili litafutiwe fedha za kutosha, bila hivyo nadhani kutakuwa na tatizo katika bajeti hii. Mimi naweza nikasema kabisa kwamba niko njia panda, sijui niunge mkono au nisiunge, ninatafakari, mpaka hapo nitakapopatiwa majibu ya kutosha, mimi ninasimama kama nilivyo na ninaomba nikae labda nitamke tu kwa muda huu sasa hivi siungi mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, naungana na wenzangu, nasema siungi mkono hoja hii, kutokana na umuhimu wa suala zima la maji katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, *World Food Program* tulikuwa tumepata shilingi milioni 104 kwa ajili ya matenki ya kuvunia maji kwenye shule zetu za msingi. Kwa masikitiko makubwa, nimepata barua tarehe 23 Aprili, wakiniambia kwamba, wametuondolea tena zile fedha kwa sababu hatukusaini *MoU*.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji anisaidie hili, siyo kweli kwa sababu *MoU* hii hapa, siku waliyotuletea na siku waliyosaini wao tarehe 28 Machi, siku hiyohiyo Mkurugenzi alisaini na aliirudisha. Sasa kama wamei-*misplace* wao, ni suala lingine. Maamuzi waliyofanya hayakunifurahisha na mimi mwenyewe nikitoka hapa nadhani nitamtafuta ili nimwonyeshe vitu hivi.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria, *KASHUWASA*, wanafanya kazi nzuri sana katika Mkoa wa Shinyanga na maeneo yote unapopita Mradi huu. Tatizo lililojitokeza ni kwamba, kuna tatizo baina ya *KASHUWASA* na *SHUWASA; KASHUWASA* wanaidai *SHUWASA* shilingi milioni 900 na kuna shilingi milioni 200, *almost* 1.1 *trillion*, mpaka hivi sasa *SHUWASA* wanashindwa kuilipa. Sasa udhaifu huu uliojitoeza umeifanya *KASHUWASA* kutokufanya kazi vizuri katika kuwaletea maji Wananchi wa Shinyanga na Kahama.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba sana, udhaifu huu unawaletea matatizo makubwa Wananchi wa maeneo yale, hasa Jimbo la Solwa, pamoja na Wananchi wa Shinyanga Mjini. Serikali ifikirie kuvunja vyombo vyote hivi na kutengeneza chombo kimoja tu, ambacho kitakuwa *responsible* katika masuala yote ya kukusanya maji, kukusanya fedha au kodi wanayolipa wanaotumia maji haya ili sasa fedha zile zisipitie kwenye mikondo mingine.

Kuwe na Bodi moja na kazi hii ifanyike *SHUWASA* ndiyo wanaochukua fedha na mpaka sasa hawajawalipa *KASHUWASA. KASHUWASA* wanashindwa hata kuendeleza huu Mradi, inakuwa tatizo kubwa kweli na hii inapelekea hata Wananchi wa Jimbo la Solwa, ambao wamepitiwa na Mradi huu kusubiri kwa muda mrefu, kuona kwamba sasa Mradi hatuupati na huduma imekuwa mbaya kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, alitazame hili, tatizo liko *SHUWASA*. Kuna Mradi ambao sasa hivi Serikali inaufanyia upembuzi yakinifu kutoka Kahama kupitia Tinde kwenda Nzega. Ninaomba sana kutokana na hii hali iliyojitokeza ya awamu ya kwanza na awamu ya pili kwenye Mradi huu wa Kahama kuja Tinde na Nzega, kusiwepo na awamu ya pili. Wanapofanya upembuzi yakinifu wafanye pamoja na vile vijiji vilivyopo ndani ya kiliometa 12, navyo vipate maji kwenye awamu moja hiyo hiyo na Mradi huo huo, siyo tena tutapitisha bomba, baadaye tena Mradi wa pili, imetuchukua zaidi ya miaka minne sasa hivi tangu Mradi huo utoke Helele kuja Solwa, kuja Shinyanga na kwenda Kahama, miaka minne hii tunasubiria maji ya awamu ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ya Ziwa Victoria, uwezo wake ni lita milioni 120, sasa hivi maji yanayotumika ni lita 17 milioni tu, utaona ni *percent* ndogo sana ya *capacity* ya maji ambayo mashine ile inaweza ikahudumia katika Mikoa yote hiyo inayopitiwa na maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali na leo Waheshimiwa Wabunge kwenye *Party Caucus* ni suala hili hili la maji. Ziongezwe fedha ili Wananchi wa maeneo yote katika Tanzania hii waweze kunufaika na maji na hasa Mradi huu wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Hakuna msalie Mtume, mimi nasema *no*, tunataka fedha za kutosha, tumechoka na ukizingatia hili limo hata kwenye ahadi za Rais. Mpaka hivi sasa fedha tulizopata ni shilingi 4.8 bilioni, ukitazama gharama zote hizi ni kama vijiji kumi tu vya mradi mzima wa Ziwa Victoria; hivi ni kweli?

Tupunguze fedha kwenye matumizi ya kawaida, ambayo tumechukua mkopo wa shilingi trilioni 1.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hebu tukamue kule kama tunakula vitumbua vinne tule kitumbua kimoja tu, safari nne tunywe safari moja tu, lakini hii tuokoe hali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi sina majibu kwa Wananchi wangu zaidi ya kusema wasubirie tuone Bajeti hii itasemaje katika Miradi yao.

Mheshimiwa Spika, maji ya *World Bank*, nilipouliza swali langu la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Maji, hakulijiu, sasa atakapo-*wind up* nataka nijue; kuna *documents* zetu, kuna Mkataba wetu katika Halmashauri yetu ya Shinyanga Vijijini.

Katika Mradi wa Didia na wa Mshepo, ambao mpaka sasa inasubiriwa kusaini kwa maana ya kumpata mshauri mwelekezi. Sasa huyu mshauri mwelekezi ni nani na hili suala la ushauri uelekezi mbona linachukua muda mrefu na unachukua fedha nyingi? Hivi Wizara wanakosa nini kuleta majibu ya haraka haraka na kama suala liko *World Bank*, basi tunaomba majibu au myafanyie kazi. Huu Mradi uanze kazi, kwa sababu Kata ya Didia, Kata ya Mshepo, Kata ya Itwangi na Kata ya Tinde, sasa hivi ni Kata ambazo Wananchi wanakuwa wengi, maji yamekuwa ya shida. Nikienda kufanya ziara yangu kule katika Jimbo la Solwa, katika watu kumi wanouliza maswali, watu wanane wanauliza maswali ya maji. Hatuna majibu nayo zaidi ya kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kwenda kutatua tatizo hili la maji.

Mheshimiwa Spika, tunamsaidia Mheshimiwa Waziri wa Maji hapa na nyumba hii yote kwa pamoja bila kujali vyama vyetu, tusimame kuona angalau shilingi bilioni 300 nyingine zinaongezeka kwa ajili ya Miradi hii ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono ule Mfuko wa Fedha ambazo Wizara ya Maji imeuunda kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya kutatua tatizo hili la maji. Ushauri wangu katika ule Mfuko, tusiende tu kwenye masuala haya ya kutoa

shilingi moja kwenye maji au sijui mnafanyaje, kuna makampuni ambayo katika utafiti uliofanywa, makampuni ya madini, makampuni ya simu, hivi tukitengeneza tu *percent* fulani kwenye makampuni hayo kwamba wanapolipa kodi katika fedha au katika mazungumzo ya simu, shilingi moja au shilingi mbili tu kwa sekunde, basi Mfuko huu utapata fedha nyingi sana na hata katika mjadala mzima huu wa maji kwa kweli utafika mahali tutakuwa hatuna matatizo makubwa sana ya kupata fedha za maji.

Sasa hivi katika Jimbo la Solwa tatizo bado ni kubwa, tunahitaji visima, kuna upungufu wa visima zaidi ya 100 na hapa ninaposema, sina namna yoyote zaidi ya Serikali kutusaidia. Mfuko huu mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuuharakishe ili ukafanye kazi vizuri na mtoe fedha za kutosha.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Wizara ya Maji mwaka jana na mwaka huu, tulipitisha fedha kwa ajili ya kupata Mradi wa Maji, 2010/2011 au 2011/12, ukitazama mwenendo mzima hapa, hakuna fedha zozote walizopata zilizoidhinishwa na Bunge. Mwaka 2000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Kitu gani, aah, sawa, si maoni yake jamani vipi! Mheshimiwa Lusinde, Mheshimiwa Natse na Mheshimiwa Anna MaryStela Mallac atafuatia.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE**: Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru Mungu kupata fursa hii ya kuzungumza ndani ya Bunge lako tukiwa na mjadala unaohusu maji.

Mheshimiwa Spika, nianze na msemo unaosema; kwenye miti mingi hakuna wajenzi. *(Makofi)*

Watafiti wengi ambao wamewahi kutafiti masuala ya maji, wanaitaja Tanzania kuwa ni nchi mojawapo yenye maji mengi sana. *(Makofi)*

Tuna maji mengi sana kwenye ardhi yetu, lakini tunashindwa kuyatoa hayo maji tuweze kuyatumia, ndiyo maana nimetumia msemo kwenye miti mingi hakuna wajenzi.

Tutazungumza sana hapa, tutajaribu kumhoji Profesa na Dokta; ni kweli kwamba, wana elimu kubwa, lakini elimu yao haiwezi kusaidia kama hawana fedha. Kwa hiyo, hapa tufanye kila linalowezekana, kuwasaidia wapate fedha ili waweze kusimamia hiyo kazi, lakini tukianza kuhoji tu, mbona wewe Profesa, mbona wewe Dokta, tunao Madaktari wengi na Maprofesa wengi wameshashindwa Urais zaidi ya mara tatu, lakini bado tunawaheshimu. Kwa hiyo, kuwa Dokta au Profesa haisaidii kama huna nguvu za kiuchumi za kuweza kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la maji, Wataalam wa Afya wanasema, tukimaliza au tukiweza kufika asilimia 80 kuwapatia Wananchi maji safi, tutakuwa tumepunguza Bajeti ya Wizara ya Afya kwa kiwango kikubwa sana; kwa sababu maradhi yote yanayosababishwa na ungonjwa wa matumbo yataondoka, kama tu Wananchi watakuwa na maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza suala la maji, hapa tusiingize siasa, tuzungumze kwa ukweli hoja nzito iliyoko mbele yetu. Katika Jimbo la Mtela, tuna vijiji zaidi ya 40, Wananchi wanakunywa maji pamoja na ng’ombe. Ukipita Fufu, Manzase, Mlodaa, ukipita maeneo yote hayo ambayo ni barabara kuu mnapita Waheshimiwa Mawaziri, mtakutana na hali mbaya sana ya maji na kila tukija kwenye Bajeti hapa tunakuta orodha tu na sasa hivi Mheshimiwa Waziri ulikuwa umetupatia, tusingeangalia kwa makini, kila Mbunge kuna orodha ya vijiji vyake, yaani hapa kila Mbunge angesoma angekuta orodha imeorodheshwa angejua mwaka huu goma limo, kumbe hakuna maji, ukija kwenye Bajeti unakuta fedha hazipo. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, tukusaidie, mimi niombe kusema kwamba, tukitoka hapa, Kamati ya Bajeti ikutane, wala sitaki kuelekeza sijui ni *OC* sijui ni wapi, ninyi mnajua namna ya kwenda kufanya, muwaongezee fedha hawa Waheshimiwa Mawaziri ili waje watugawie hapa tuweze kupata visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ingekuwa vyema Bunge lako likawa na utaratibu wa kupata mrejesho ulio sahihi; kwa mfano, kabla ya Bajeti ya Maji kusomwa, kwanza, tungeelezwa ni Miradi gani imetekelezwa; hiyo ya Benki ya Dunia, vijiji vingapi vimepata maji, wapi wanakunywa maji, ili tuelewe kwamba kumbe kazi iliyobaki ni kutoka hapa kwenda mbele zaidi. Tukiwa tunafanyia kazi ujumla ujumla hivi, hatuwezi kujua wapi kuna maji, wapi watu hawajapata maji, tutakuwa tunasikia tu *World Bank, World Bank.*

Katika huo Mradi wa Vijiji Kumi, ingekuwa vyema Waheshimiwa Wabunge wote tupate orodha ya vijiji ambavyo tayari wanakunywa maji, tungejua kwamba ahaa, kumbe katika vijiji vyote hivi, limepunguzwa kiasi kadhaa. Tukizungumza kwa ujumla wake, tutakuwa tunapoteza muda bure. Maji yenyewe ya Benki ya Dunia gharama yake ni kubwa mno, unakuta mradi wa kijiji kimoja shilingi milioni 488 wakati unaweza kuzigawa zile ukapata maji katika vijiji vinne.

Maji yanachimbwa kwa gharama kubwa, yanasambazwa kwa gharama kubwa, bila sababu yoyote ya msingi. Kwa hiyo, niishauri Serikali, hakuna sababu, kama wametupa zile fedha, namna gani ya kuzitumia watuachie sisi na Halmashauri, tuangalie kwamba ukikaa mahali kwenye kijiji chako, gharama ya shilingi milioni 100 unaweza kupata maji ukatumia shilingi milioni 100 badala ya shilingi milioni 488. *(Makofi)*

Tunapoteza muda bure, tunayo maji kila sehemu yamechimbwa yamefunikwa, watu hawayatumii, ukija kuiangalia Bajeti, kila kijiji milioni 400, wakati wenyewe tukichimba maji hata kwenye visima vyetu binafsi, tunayapata kwa fedha kidogo sana. *(Makofi)*

Utaratibu huu tunawezekana kabisa na sitegemei kwamba hata matumizi yetu ya ndani ya namna ya kupangua Bajeti yetu ili itoshe vijiji vingi, nalo Banki ya Dunia wanatusimamia, itakuwa ajabu sana. Wao wametupa fedha sisi tuchukue fedha hiyo tuigawanye.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalotaka kulizungumza hapa ni mtiririko wa fedha kutoka Hazina. Wizara ya Maji haina kipaumbele chochote, ukienda kutazama pale kila siku unawaona akina Mheshimiwa Profesa Maghembe wako Wizara ya Maji wanaomba fedha. Hivi wenzetu wa Wizara ya Fedha hamwoni umuhimu wa maji wa sababu ninyi mnakunywa maji? *(Makofi)*

Mimi nataka kutumia fursa hii kuwasihi Watanzania, kuanzia leo, ziara iwe ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, iwe ya Mbunge au ya Spika, msimuwekee maji ya chupa, wekeni maji mnayokunywa ninyi. Maana hii tabia ya Watanzania wakishaona mkubwa umekuja pale wananunua Kilimanjaro, wewe mkubwa unajisahau unafikiri wale wana maji kumbe hawana. Piga jagi, weka pale kipeo chako, mwekee pale Mzee Pinda, akiona mabaya basi ataenda kuhakikisha analeta maji pale ya kunywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nawaomba Watanzania walizingatie sana wala viongozi wa ngazi ya chini wasiogope kwamba watafukuzwa kazi, hawawezi kufukuzwa, sisi Wabunge tutawatetea. Leteni maji hayo hayo machafu mnayokunywa kwenye meza za Mawaziri ili na wao wanywe, wakishindwa waende wakahakikishe wanaleta maji safi kwa ajili ya nchi nzima. *(Makofi)*

Hatuwezi kukubali utaratibu huu, kila mtu ukifanya ziara wanakuwekea maji ya Kilimanjaro wakati wenzako wanakunywa maji machafu, kuna watu wanaoga siku wakisikia ziara ya Waziri tu; haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la aibu sana, kama leo Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere angefufuka, angeshangaa sana, mabwawa mengi ambayo

waliyachimba leo yamefukiwa, hata kufukua tu tunashindwa! *(Makofi)*

Ukitembea katika Vijiji vya Mlowa Bwawani, Idifu, Mvumi Mission, Mkulabi, utakutana na mabwawa mengi yaliyochimbwa enzi zile za Mwalimu. Unajiuliza hivi Mwalimu aliwezaje wakati ule na uchumi ulikuwa mgumu na sisi tunashindwaje! *(Makofi)*

Tumekuwa tunapata habari hapa, tumepigana wee, tumetumia muda mrefu kwenda Wizara ya Maji kuomba Bwawa la Sasajila likamilishwe pale, lakini hakuna lolote, kuna ubabaishaji mtupu kwa watendaji wetu. Hebu tuangalie, tunaweza tukafikiri adui mkubwa wa CCM ni CHADEMA, kumbe adui mkubwa ni Watendaji waliomo ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Tutapoteza muda bure, twende tukapambane na baadhi ya Watendaji wasiokuwa waaminifu ili Wananchi wetu wapate maji.

Mheshimiwa Spika, niombe sana maji katika vijiji ambavyo tangu Uhuru havijawahi kupata maji. Kijiji kama cha Igandu, Nghaelezi, Chinoje**,** Chanhumba, hawajawahi kupata maji tangu Uhuru. Unashangaa hatujawahi kuwaweka hata katika orodha; kwa mfano, nimeona kwenye orodha ya kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri wa Maji, ametaja kuna Kijiji kinaitwa Chinoje kwamba kuna Mradi wa Maji wa *World Bank.*

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri, pale wamechimba zaidi ya mita 120 hawakupata maji. Kwa hiyo, hiki hakipo kwenye mpango wowote, kwa sababu maji pale chini hayapo, labda twende mbali zaidi. Kwa hiyo, ni vyema tukawapa taarifa sahihi ili wakati mnatusaidia mtusaidie. Nenda katika Kijiji cha Mvumi Mission, kina watu 21,000, lakini pale tangu Uhuru hakuna kisima cha maji kilichochimbwa na Serikali. Maji yaliyoko pale ni kidogo ya Kanisa. Sasa Kanisa lina miradi mingi pale; wana Shule yao ya *DCT*, wana *High School*, wana shule ya wenzetu wenye

ulemavu wa macho, wana vyuo vitatu pale. Kwa hiyo, unakuja maji yao hayawatoshi wao wenyewe, sembuse kuwapa Wananchi; tuna matatizo makubwa sana ya maji.

Tunawaomba sana, Mheshimiwa Spika na wewe vilevile tunajua nguvu yako ya Kiti ni kubwa, unaweza kuwaambia hawa leo wakutane waongeze fedha ili na Jimbo lako nalo nalisemea lipate maji. Kwa sababu shida ya maji ipo kuanzia kwenye *back bencher* hadi kwa Waziri Mkuu.

Tunapozungumzia vipaumbele, zipo Wizara wakati mwingine tunaweza tukasema mwaka huu tulipe mishahara tu Wizara hii, fedha zote za maendeleo tupeleke kwenye maji. Tuangalie vipaumbele vya Wizara, tukitaka kufanya kazi ya maji mwakani, tabu yake ni kwamba, hawa wenzetu watafikiri tunafanya kwa ajili ya uchaguzi, kwa hiyo, tufanye sasa.

Tufanye sasa watu wetu wapate maji. Watu wakishapata maji na nikwambie Mheshimiwa Spika, tukipata maji tutaokoa nguvu kazi kubwa sana ya Taifa, kwa sababu akina mama wengi badala ya kufanya kazi ya kuhangaika kutafuta maji, watafanya kazi ya kuzalisha. Wataungana na wenzao kwenda kuzalisha mali badala ya kuhangaika kutafuta maji. Hapa Dodoma hatuna mto unaotiririka maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, tena na magonjwa yatapungua.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Siungi mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, nashukuru. Sasa nimwite Mchungaji Natse na Mheshimiwa Anna Mary Stella Mallac, dakika tano tano.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nitumie dakika chache nilizonazo kujikita katika Jimbo langu la Karatu. Kama wengi

walivyosema, Bajeti hii ya Wizara ya Maji haitoshi na Serikali haina nia ya dhati kuhakikisha Wananchi wake wanapata maji, kwa sababu ukiangalia vitabu vya maendeleo, sehemu kubwa ni fedha za nje na siyo za ndani na katika Halmashauri nyingi, hakuna Bajeti kwa ajili ya maji. Maji wanasubili wafadhili walete fedha.

Nije kwenye Miradi ya *World Bank*; ni kweli ni Miradi ambayo ipo hoi na haitatusaidia. Fedha nyingi, shilingi milioni 400 *plus*, haiwezi kuleta maji kwa kijiji kimoja, kwa sababu asilimia kubwa ya fedha zile zinaliwa na wakandarasi. Hii tabia nafikiri tuiache kama Serikali, wakandarasi hao waogopeni kama ukoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 18 Machi, 2013, Mheshimiwa Waziri Profesa Maghembe, alifika Karatu kwa ajili ya kero ya maji na akatoa kauli nzito kwamba, Karatu tumesikia kilio chenu na ni kwa mara ya kwanza nafikiri Serikali imekumbuka kupeleka maji Karatu. Akasema wataweka pampu kwenye kisima ambacho kipo tayari, watachimba visima viwili, watajenga vioski kumi na kujenga matenki. Ndani ya siku kumi kazi hii itakuwa tayari. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha anipe majibu maana hata sasa hakuna kinachoendelea pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kutunza vyanzo vya maji. Hili ni muhimu sana, pasipo kuonea aibu mtu yeyote awaye, vyanzo vya maji vitunzwe kwa gharama zote. Ninakumbuka tunayo mabonde mengi ambayo kimsingi yanahitaji kuangaliwa, siyo kukaa ofisini, hawa watu wa mabonde hasa Bonde la Kati, waende kwenye mabonde waangalie skimu zinakuwaje.

Katika Bonde la Eyasi, matatizo yaliyoko pale ninaweza kudiriki kusema kwamba, yanasababishwa na watu wa Bonde la Kati**,** wanatoa maagizo toka ofisini, hawafiki kwenye *site*. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, ufike kwenye Bonde la Eyasi kwenye chanzo cha Kandend uangalie, maana maji ni uhai wa Wananchi wote wa eneo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuweka kumbukumbu sawasawa, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, alilipotosha Bunge lako na Wananchi wa Tanzania; Jimbo la Karatu linaongozwa na CHADEMA na katika Mabaraza ya Katiba, Jimbo lile limepewa *members* 75, CHADEMA ina *members* 45, CCM na wengine waliobaki, ilishangaza kudanganya Bunge na Wananchi kwamba hata kule Karatu CCM ilishinda; *shame to him!*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, naomba uondoe hayo maneno yako ya mwisho.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Ahsante, naondoa.

Kwa kuwa tumekubali Vyama Vingi, twende pamoja kwa nchi hii maana ni nchi yetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni suala la uvunaji wa maji. Naiomba Serikali iwekeze katika kuvuna maji hasa katika Taasisi zetu kama shule za sekondari na msingi, hospitali na zahanati. Tuvune maji kwa ajili ya mahitaji ya binadamu na hili linawezekana, kujenga matanki, kuweka *gutters* katika shule zote na taasisi zetu zote, kwa namna hii tutasaidia sana shida kubwa ya maji inayowakabili Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli bajeti hii inahitaji kuongezwa kama wengi walivyoomba, naiomba Serikali irudi tena ikae, kabla ya kupitisha watuletee kitu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anna MaryStella Mallac dakika tano.

**MHE. ANNA MARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunipa afya siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa narudia maneno waliyoongea wenzangu kwamba maji ni kitu muhimu sana

kuliko hata KILIMO KWANZA, kwa sababu KILIMO KWANZA hakiwezi kutekelezwa kama hakuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea shida ya maji siyo kwamba tunahitaji maneno matamu kuyasikia masikioni na mipango isiyokamilika. Ninaomba Waziri wa Maji, aelekeze macho yake ya huruma katika Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa. Wanakatavi watanishangaa sana ikiwa nitaunga mkono bajeti hii ya maji pamoja na Wanarukwa. Kwa kweli tunajiona kama ni watu ambao tumetengwa sana, naomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Maji, awahurumie sana Wananchi wa Rukwa na Katavi, ambao wapo pembezoni mwa nchi, ambao tupo nyuma kwa kila kitu kuanzia barabara, maji na elimu. Vitu vyote hivyo tumesahaulika sana. Kwa hiyo, naomba hili suala la maji alipe kipaumbele hasa vijijini. Siwezi kuongelea sana mjini, naongelea vijijini ambapo ndipo kuna wazalishaji wakubwa, asilimia 80 ya Wananchi wako kule wanahangaika sana kutafuta maji. Jamani wanawake wa vijijini wanahangaika sana, Mheshimiwa Waziri wa Maji hebu waonee huruma wanawake wale.

Leo hii Tanzania miaka 52 tangu tumepata Uhuru, bado ni wa kuchota maji kwa kichwa tena kuchota kwa kata kwenye madimbwi, maji ambayo yamebadilika rangi na ya kijani yanateleza kama mlenda; jamani! Wananchi wanakunywa maji Mheshimiwa Waziri kama togwa!

Mimi nimekuwa natembelea sana vijijini, naona aibu ninapowazungukia Wananchi wananiandalia chakula halafu wananiwekea maji mazito kama togwa. Kwa kuwa wanaokunywa ni Wananchi wenzangu na mimi nalazimika kunywa huku naomba Mungu nisaidie nisipange foleni nyumbani ya kuingia sehemu muhimu. Jamani, wahurumieni sana Wananchi wa vijijini.

Kuna vijiji nilivyovitaja mwaka jana na mwaka huu sitavirudia, kwa sababu nitakuwa napoteza muda dakika ni chache. Naona Serikali imevipanga kwenye kitabu chako kwamba vipo kwenye mpango wa vijiji kumi. Nitashukuru kama mpango huo utatekelezeka, kwa sababu Serikali

imekuwa na maneno mengi kama ni mama mpaka watoto tutakuchoka.

Naomba Wananchi wa vijijini waangaliwe hasa kwa maji, siwezi kuvitaja vijiji itakuwa ni kurudia. Kijiji cha Majimoto, Kata ya Majimoto, naomba uwakumbuke sana Mheshimiwa Waziri, watu wale wana adhabu, wanakunywa maji ya moto yanayofuka moshi. Hebu niwaulize Wabunge wenzangu kwamba; leo hii tuambizane kuanzia kesho wote tunapokula chakula tuanze kunywa maji ya moto kama chai yanakidhi kumaliza kiu? Ndiyo wenzetu Majimoto wanakunywa maji hayo ambayo yanafuka moshi, ni maji ya kunywa hayo na ukikuta mwananchi anayekunywa maji ya baridi amenunua, debe la lita 20 amenunua kwa shilingi 2,000 au 1,500 na maji hayo wanunuzi wanayatoa kilomita nane kijiji kinachoitwa Mamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo...

*(Hapa kengele Ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika tano zimeisha mama. Ahsante. Sasa nitamwita msemaji anayefuata, Mheshimiwa Dkt. Kebwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, atafuatiwa na Mheshimiwa Aliko Kibona.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na mimi nichangie katika Wizara hii nyeti ya Maji. Nianze na ninaomba nieleweke kwamba, siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja kwa sababu zifuatazo:-

Nashukuru Mheshimiwa Waziri anafahamu historia ya Bwawa la Manchira. Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, anafahamu Bwawa la Manchira. Mheshimiwa Profesa Mwandosya anafahamu sana historia ya Bwawa la Manchira.

Mheshimiwa Spika, kilichofanyika katika Bwawa la Manchira pale Serengeti, Mji wa Mugumu, unapata maji kutoka katika Bwawa hili. Tunaishukuru Serikali kwani gharama kubwa sana imetumika, lakini Mradi umeishia njiani, haiwezekani maji yapatikane ambayo hayatoshelezi, lakini mfumo wake ule wa mtandao haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi, Wanaserengeti kilio kikubwa ni kule kufananishwa sasa na sisi tuishi kama wanyama walio mbugani pale. Haiwezekani tupewe maji ambayo hajatibiwa. Hii ni kinyume kabisa hata na ubinadamu, yale maji kama hayatibiwi; hivi ilikuwaje Rais Jakaya Kikwete alipelekwa pale kufungua Mradi ule? Nina hakika labda alidanganywa, sidhani kama angefahamu yale maji angekwenda kukata utepe, hayatibiwi halafu aruhusu Watanzania, Wanaserengeti na Wanamugumu, wayanywe yale maji. Tunaiomba Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, kunapokuwa na ziara hizi za viongozi mbalimbali, vilevile ni sehemu ya kujionea uhalisia, kwa nini hawa viongozi wanaotembelea Miradi mikubwa kama hii ya Kitaifa wanadanganywa? *(Makofi)*

Hivi ni Mawaziri wangapi ambao walishatembelea Bwawa la Manchira? Imekuwa kama ni Mradi wa Maonesho, kila Kiongozi wa Kitaifa anayetembelea Serengeti ni lazima apelekwe Bwawa la Manchira, kufanya nini kama Mradi huu haukamiliki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni Serikali iongeze fedha na ndiyo sababu mimi siungi mkono. Iongezwe fedha, hili ambalo linazungumzwa la shilingi bilioni 30 kupelekwa Mwanga ni sehemu ya mradi wa utekelezaji kama ambavyo Bwawa la Manchira linatakiwa lipewe fedha. Fedha hizi zikiongezeka, naomba Bwawa la Manchira, mtambo wa kusafishia, ile *Water Treatment System* uwekwe, fedha ambayo ilikuwa imekadiriwa, shilingi bilioni 17.5, pamoja na mtandao wa kwenda kwenye vijiji vya sehemu ya Manchira, Kwamichanga, Miseke, Bwitengi na sehemu zote za mtandao zikiwemo Kibeo na Kisangura, ni vizuri utazamwe. Fedha ambazo zilikuwa zimekadiriwa hizo shilingi bilioni 17.5 basi

zingekuwa zinatolewa hata kwa awamu. Kwa hiyo, fedha hii ikiongezeka kama zile shilingi bilioni 30 pale Mwanga zitaendelea kuwa hivyo, mimi sitaendelea kuunga mkono. Ni vizuri keki inapokuwa ndogo basi kila mtu apate kidogo, lakini suala hili ni la ubinadamu, Wananchi wa Serengeti wanapewa maji ambayo hayatibiwi.

Kuna usemi unasema kwamba, kinga ni bora kuliko tiba. Kwa takwimu ambazo zipo kidunia, ukieleza vizuri katika suala la mazingira na suala la maji, asilimia 80 ya magonjwa ya kuambukiza yanatoweka na ndiyo sababu hata wenzetu kwa nchi ambazo zimepiga hatua kidogo walifanya hivyo, hawalii mambo ya matumbo, kuharisha na nini havipo kwa sababu ya suala la maji. Ukiangalia mwanafalsafa mmoja, Wiliam Fisher, ambaye alijaribu kutengenisha haya magonjwa kutokana na matatizo ya maji ikiwemo *water related, water waste, water based* na kadhalika. Kwa njia hii ndiyo ambayo ilisaidia kuondokana na maradhi haya ya kuharisha na kuhara.

Kwa hiyo, naomba sehemu ya pili, mradi mkubwa wa maji ambao unaendelea pale Musoma, pampu yake ikikamilika inaweza kusukuma kwa *gravity* mpaka kilomita 50, ambayo inakuwa imebakia kilomita kumi kuingia Serengeti. Kwa hiyo, ni vizuri tutumie fursa hii kusudi mtandao ule wa maji kutoka Ziwa Victoria usambae mpaka Serengeti, ni kiasi cha kuweka pampu ya kusogeza nguvu kwenda Wilaya ya Serengeti, ndiyo njia pekee ya kusambaza maji ya Ziwa Victoria. Kwa nini tuyaachie maji haya ambayo asilimia 70 ya maji yanayongia Ziwa Victoria yanatokea Tanzania? Kwa hiyo, ni vizuri fursa hii nzuri ambayo tunayo tusiiachie, maji yale yanaenda katika nchi za wenzetu wanajenga mabwawa na kufanya kazi nzuri za kimaendeleo, ikiwemo Misri na Sudan, maji yale yanatokea kwetu na tunayazalisha sisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba suala hili lifanye kazi ya kimkakati, wataalamu ambao wako Wizara ya Maji tumieni fursa hiii ili utaalamu wenu ufanye kazi ambayo itawasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Jambo lingine ninaloshauri ni kwamba, miradi ya Benki ya Dunia, tunaiita hivyo lakini ni sehemu ya *support* ya Benki ya Dunia, haijafanyiwa *evaluation,* nina hakika, ingekuwa imeshafanyiwa tathmini, sidhani kama tungeendelea na utaratibu huu. Haiwezekani Mradi unakuwepo miaka kumi shughuli haziendi halafu bado tunakwenda; nini maana ya *monitoring and evaluation*? Ufuatiliaji na tathmini unakusaidia kuchukua uamuzi kwamba, *are you on truck;* yaani unakwenda kulingana na mpango wenyewe ulivyo; kama hauko *on truck* unabadilisha utaratibu.

Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, ni vizuri tuachane na mambo ya visima ambavyo vinatumia gharama kubwa katika Mradi huu. Tukijielekeza katika mabwawa inakuwa ni *multipurpose;* kivipi? Utapata maji kwa ajili ya mifugo, kwa ajili ya Ndama wakiwemo, unatengeneza *trough* halafu unaweka na *DP* kusudi maji yale yatumike kwa ajili ya mifugo na binadamu katika uwanja mpana. Kwa hiyo, ni vizuri hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, naomba tuwekewe mita katika Mji wa Mugumu. Siyo vizuri mtandao wa maji ambao upo kwa watu wachache wenye mabomba katika maeneo yao halafu unakuta Wananchi wengine wanakwenda kuchota maji pale wanalipishwa kwa sababu hakuna mita. Kwa hiyo, ni vyema Wizara ikae vizuri ifanye ufuatiliaji wa karibu na isimamie ili kama ni Serikali kutoa *seed money,* iwepo kwa ajili ya kununua mita, hii itasaidia kuongeza wigo wa ukusanyaji wa fedha kuliko watu wachache wanahodhi maji halafu wao ndiyo wanakuwa wafanyabiashara wakubwa wa maji kuliko matumizi ya jamii. Hii itasaidia kupiga hatua katika usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ninachokiona kikubwa cha msingi, Miradi hii ambayo tunaanzisha halafu tunaishia katikati, haitusaidii sana. Katika Bunge mwaka juzi niliuliza kwamba Bwawa lile la Nyamitita hivi limeishia wapi? Jibu nililopata ni kwamba, zimepangwa fedha shilingi milioni 700. Je, fedha hizo mpaka leo zipo wapi? Mradi umesimama hakuna kinachoendelea. Katika kujibu hoja, Mheshimiwa

Waziri anapokuja kuhitimisha, aje na majibu ya kueleweka ya kuwasaidia Wanaserengeti. Hii ndiyo njia pekee ambayo tutaachana na Miradi hii ambayo tunaanzisha halafu inaishia katikati, *at the end of the day,* inakuwa *very expensive,* kwa sababu kulingana na muda unavyokwenda na thamani ya fedha nayo inabadilika, ni dhahiri itakuwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa cha msingi ninachopenda kushauri Kamati ya Bajeti hii ambayo imeanzishwa, tuone kazi yake, *performance* yake ikoje, ili wenzetu warudi wakawatafutie fedha. Nimepitia katika vitabu vyote, Wizara mbalimbali maeneo yapo mengi ya kubana matumizi, haiwezekani vitafunwa na chai inachukua *billions of money!* Fedha hizi nyingine zipunguzwe na fedha nyingine za matumizi ya kawaida. Ukienda katika ile 250300 unakuta kifungu kile ni *perdiem domestic,* kinachukua fedha nyingi kwelikweli; ni vizuri maeneo mbalimbali yaangaliwe. Wataalamu ambao wapo katika Kamati ya Bajeti wapitie upya. Hii itasaidia.

Kikubwa na cha kushangaza ninachokiona, tumepigia kelele kwenye suala la maji na nina hakika kama utakubali tufanye majaribio, basi maji yasipatikane katika maeneo haya ya Bunge ikiwemo Bunge hapa tulipo, japo kwa siku moja, kelele tutakazopata na maandamano ya Wabunge ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante, kwani unatakaje mgawana matatizo? Tunaganga huko yaliko.

Sasa nimwite Mheshimiwa Selemani Jafo na Mheshimiwa Aliko Kibona ajiandae.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, mchana wa leo na mimi kupata nafasi.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi kwetu kule kuna kitu kinaitwa timbwili, ukiona kila Mbunge hapa anajadili suala la maji kwa uchungu basi ujue suala hili ni kubwa sana. Jambo hili kwa nini maji? Nikinukuu vitabu vya dini kwa Lugha ya Kiarabu, Mwenyezi Mungu anasema: *"Wahuwa radhi haraka-mina-l-imai-bashara, farajaharahum nasaba waswila wakana-rabuka kadira".* Kwamba, hakika Mwenyezi Mungu ndiyo amemwumba mwanadamu kwa maji, akamjalia ujungu wa damu na udugu wa kuoana. Kwa hiyo, ndiyo maana unaona kila mtu anaguswa na suala zima la maji, ndiyo maana naomba Wabunge wote kwanza tuache jazba tuseme kwamba jambo hili ni kubwa kweli kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi kama unakumbuka siku zote nikisimama Bunge hili nalilia sana shida ya maji katika Jimbo langu la Kisarawe na sijasimama hata siku moja kuacha kuzungumzia shida ya maji.  Wananchi wangu wana shida kubwa kwelikweli ya maji na hili nitaendelea kulisema ndani ya miaka yangu yote mitano, shida ya maji Wilaya ya Kisarawe na ndiyo maana vipaumbele vyangu vitano katika Jimbo langu la Kisarawe ni shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Mwenyezi Mungu anasema usipomshukuru binadamu mwenzako hata Mwenyezi Mungu utashindwa kumshukuru. Naishukuru sana Serikali, imenisikia kwa shida ya maji Wilaya ya Kisarawe. Juzi tumepata shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuweka miundombinu katika visima vitano vilivyokamilika hivi sasa. Katika Kisima cha Kihara, Kikwete, Mradi wa Mafizi, Kisima cha Boga na Msanga; kwa kweli Wizara nawashukuru sana kwa sababu watu wa Kisarawe wana shida kubwa ya maji.

Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana.  Katika ukurasa wa 15 na mpaka nikapiga simu kwa *Engineer* wangu wa Wilaya, nashukuru sana kupata ufadhili kutoka China kwa visima 20.  Nimepata taarifa pale Wilaya yetu ya Kisarawe, ndugu zangu Wanabunge hili, Kisarawe tunataabika kweli shida ya maji. Serikali imefanya hili kwangu mimi na mimi kama binadamu lazima niridhike niseme kwamba, haiwezi

kumaliza shida yote ya maji lakini angalau kidogo tumeanza kupiga safari hii. Nina imani kwamba, taratibu Wanakisarawe mwisho wa siku tutapata nafuu katika shida ya maji.

Nakumbuka juzijuzi ofisi yako ilipata taarifa kwamba, wakati Mheshimiwa Mwandosya akiwa Waziri, tulipata Mradi wa Maji wa shilingi milioni 540, Mji wa Kisarawe ulipata shida kubwa sana ya maji. Mradi ule umeanza kufanya kazi vizuri, lakini mota yetu ikawa imeungua pale, bahati mbaya maji kidogo yana changamoto kubwa kwa sababu ya kuwepo kwa madini mengi sana ya *iron*. Nadhani Ofisi ya *DAWASA* wameshapata taarifa hii, naomba ndugu zetu wa *DAWASA* washirikiane na wataalamu wetu pale Wilayani, kuhakikisha kile kiwango cha madini ya chuma kinarekebishwa ili watu wangu wa Kisarawe waweze kupata maji mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunazungumza shida ya maji, lakini tujue kwamba, ndani ya miaka kumi iliyopita, Tanzania imeongezeka zaidi ya watu milioni kumi. Watu milioni kumi maana yake ni sawasawa na lita milioni 250 zinatakiwa kwa siku. Ina maana kwamba, mahitaji yetu ya maji kwa Tanzania sasa ni makubwa. Hapa tuna kila changamoto kubwa ya kutafakari kwa kina jinsi gani tutafanya ili tupambane na shida yetu ya maji katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri na Ofisi yako, Serikali, naishukuru sana kwa kuweka shilingi milioni 35 kwa Mradi wa Kimbiji na Mipera ambayo Mradi huu kwa mujibu wa taratibu utasaidia Jiji la Dar es Salaam, lakini utasaidia kwa kaka yangu pale Mheshimiwa Adam Malima, Mkuranga pale, lakini na kutusaidia sisi watu wa Mji wa Kisarawe. Naomba aendelee kuweka nguvu sana Mradi wa Kimbiji uweze kukamilika. Wananchi wangu wa Mji wa Kisarawe pamoja na kwamba wanaweza kupata maji salama, lakini angalau na wao waweze kujisikia sehemu yenye amani ya kuweza kuishi.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo maana nimesema mimi nikiwa Mbunge na sehemu yangu imeguswa, lazima nishukuru. Mwaka jana tulikuwa tunapitisha bajeti ya

barabara hapa miundombinu, kwangu Kisarawe sikutengewa hata barabara moja ya lami, ukiangalia mikoa ya Kaskazini wamejengewa lami mpaka vyooni huko na watu tulipitisha ile bajeti. Bajeti hii ya mwaka huu mimi naiunga mkono na ndugu zangu wanasema sijui Mwanga, tuzungumze mambo ya Kitaifa, tukiwa tunawanyooshea wenzetu vidole wenzetu wa Mwanga na Same wale nao ni binadamu, watajisikia vibaya. Serikali yetu imetumia mamilioni ya shilingi kutoa maji Ziwa Victoria yanakwenda mpaka Tabora; mbona watu hawakusema? *(Makofi)*

Jamani Mradi wa Kitaifa lazima ugharimu pesa nyingi sana, lazima kama Wabunge tuwe na jambo moja la Kitaifa, tutakuja kubaguana kwa sababu Mikoa ya Kaskazini sisi wengine lami na mambo mengine, tutakuja kubaguana humu. Hata ukiangalia katika kitabu cha barabara, ujenzi wa barabara mwaka huu, tutaanza kushikana mashati hapa. Kuna mikoa mingine wamewekewa mabilioni ya fedha.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Tutashikana mashati Wabunge hapa, tujadili kwa pamoja kama pesa haitoshi tutafanyaje kuongeza pesa ili kusaidia Sekta ya Maji, tusinyoosheane vidole. Kila mtu anazungumzia Jiji la Dar es Salaam, ndiyo, lakini tuangalie hata *investment* ya kiasi gani pesa imewekwa Dar es Salaam kulinganisha na sehemu nyingine tunakotoka.

Kwa hiyo, tuzungumze kwa pamoja kwamba kweli pesa ya maji haitoshi, kama Wabunge tukae tutafute njia ili pesa iongezeke na Mheshimiwa Maghembe hapendi kudhalilishwa mtu mzima na Dokta wangu pale, hawapendi kudhalilishwa. Wao siyo kwamba wana pesa mifukoni, hapana. Kazi ya Wabunge maana yake kuishauri Serikali na kuielekeza na kuisimamia. Sisi Wabunge tuishauri Serikali kwamba pesa ile ni ndogo.

Jana Mheshimiwa Serukamba alishauri kwamba, tukate *OC* hata ya asilimia 15, mimi nimesema hata asilimia

kumi tutapata zaidi ya bilioni 300 au 400, tutaongeza katika Sekta ya Maji na itasaidia maji vijijini. Ndiyo maana nasema kama Wabunge, tukubaliane kwamba bajeti ya maji haitoshi. Bahati nzuri sana, nawashukuru sana Mheshimiwa Profesa Msolla, Kamati yako imefanya kazi kubwa sana kusema kwamba, bajeti hii haitoshi. Nimesikitika sana, Mbunge anasimama hapa anailamu Kamati; Kamati imejaa akina Profesa Msolla halafu mnaidhalilisha hapa! Kazi kubwa wanayofanya akina Mama Makilagi, akina Subira Mgalu na Wataalamu wamekaa wamejadili na kuishauri Serikali kwamba tuongeze shilingi bilioni 185, unasema Kamati hijafanya lolote! Kamati ndiyo imetuonesha njia kwamba bajeti haitoshi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama Wabunge, nakushauri Mheshimiwa Spika kwamba, ikiwezekana tukitoka hapa Serikali iende ikakae itupe majibu jinsi gani pesa zitaongezwa. Hakuna sababu ya kutafuta ujiko au sijui kutoa hoja, hakuna haja ya kutoa hoja hapa, hoja tunachotaka ni kwamba, Serikali ikaongeze pesa tu. Hakuna kutafuta ujiko wa burebure hapa, Wabunge wote tumesema kwamba tunataka pesa iongezeke ili Wananchi wetu wapate maji na ndiyo maana tunaiagiza Serikali kwamba ikakae ikafanye mawazo ya kina katika kutusaidia kutatua shida ya maji, wote tuna shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukitatua tatizo la maji tutakuwa tumewagusa Watanzania wote. Sote tuna shida ya maji na suala la maji ni jambo la msingi na ni jambo la kulisimamia.

Nawashukuru sana ndugu zangu wa *DAWASA,* nimepata taarifa kwamba wiki ijayo wataanza kuchimba maji katika maeneo ya Chole. Nawashauri watu wangu wa Chole ambao sasa hivi mnanisikiliza kwamba, Wataalamu wa DAWASA wakifika huko shirikianeni nao mhakikishe maji yanakwenda kuchimbwa sehemu ambayo tulikusudia kuchimba maji tuweze kupata maji.

Vilevile nawaomba Wataalamu wangu wa Halmashauri pale Kisarawe, wahakikishe hivi visima vya

Wachina vinavyokuja kule kwa kushirikiana na Serikali, viweze kusimamia kuwapelekea watu wa maeneo ya Mzenga, Malumbo na Manelomango, wapate maji katika maeneo yote ya Wilaya ya Kisarawe. Shida kubwa ni kwamba, Wananchi wetu hawawezi kupata maji.

Mheshimiwa Spika, samahani, maana nilitaka niseme Kisarawe oyee, nimejisahau nilidhani nipo katika majukwaa ya kisiasa. Ni kwamba, lazima kama Wabunge tuhakikishe kwamba, tunashikamana kwa pamoja. Naiomba Wizara, tuweze kuangalia na vilevile uharibifu wa tabia nchi umekuwa mkubwa kwelikweli. Sasa hivi takwimu zinatuonesha kwamba, kuna maeneo mengine mvua imeshuka kutoka milimita 1500 kwa mwaka mpaka milimita 780.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na ninaomba nimwite Mheshimiwa Aliko Kibona.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna msemo unasema, anayeshukuru maana yake anaomba tena. Niseme tu kwamba, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mahenge, alifika Ileje kwa ajili ya kufungua Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mbebe. Ninashukuru sana. Ninaposhukuru maana yake ajiandae ninataka kuomba tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwamba, Mradi mkubwa wa Maji unaendelea katika Kijiji cha Ruswisi na unaelekea katika hatua za mwisho. Kwa muda mrefu kila nikisimama katika Bunge lako Tukufu, nimekuwa nikitoa kilio kwa ajili ya Mji wa Isongole. Alikuwepo mama mmoja, alikuwa na mtoto mgonjwa, akasikia Yesu Mnazareti anahubiri mahali na kuponya wagonjwa. Yule mama akakimbia akamwacha mtoto wake nyumbani, alipofika akaenda moja kwa moja

kwa Bwana Yesu akamwambia mtoto wangu ni mgonjwa yu hawezi. Yesu akasema yuko wapi? Akasema yuko nyumbani. Yesu akasema nifanyaje? Yule mama kwa imani akasema sema neno tu na mgonjwa wangu atapona. Yesu akasema sijapata kuona imani kubwa namna hii.

Nimekuja kwako Mheshimiwa Waziri, nimeacha mgonjwa yuko Isongole anahitaji shilingi milioni 500, usiniulize yuko wapi, nasema sema neno tu na mgonjwa wangu atapona. *(Makofi)*

Mji wa Isongole ni mkubwa, unakua kwa kasi, pana Boda na Uhamiaji, wageni wanatoka nchi mbalimbali wanachukua vibali vyao pale ili kuendelea na safari zao kwenda nchi za Kusini mwa Afrika. Mji ule hauna maji kwa muda mrefu toka tumepata Wilaya ya Ileje hatuna maji. Maji yaliyopo yaliwekwa miaka ya 1978 na wakati wa masika yakitoka kidogo yanakuja na tope la kutisha, watoto wanakunywa maji yale hawawezi kuhudhuria masomo kwa sababu ya homa za matumbo. Mheshimiwa Waziri, naomba sema neno tu, katika hiki ambacho wenzangu wamesema kwamba, Serikali iende ikajipapase iangalie mahali pengine tuweze kupata hela ya nyongeza. Naomba uelekeze katika kuongezaongeza kila mahali usinipite na mimi, uweke nyongeza katika Mji wa Isongole. *(Makofi)*

Ninakushukuru kwa ajili ya visima vifuatavyo: Mheshimiwa Waziri ameniambia katika mwaka wa fedha ujao Serikali italeta maji katika Vijiji vya Ibaba, Shikunga, Ipande, Mtula, Chibila, Malangali, Kalengo, Bulanga, Kafule, Kapelekesi, Kikota na Sange. Ninashukuru maana yake ninaomba, nikitoka hapa ninakwenda kifua mbele, nakwenda kuwaambia Wananchi wa maeneo hayo maji yanakuja. Wakiniuliza nani amekwambia maji yatakuja? Nitawaambia Mheshimiwa Profesa Maghembe kupitia kauli yake kwa niaba ya Serikali amesema maji yanakuja katika vijiji hivyo. Ninaomba maji yafike katika vijiji hivyo ili furaha yangu na shukrani yangu kwako isije ikageuka tena kuwa lawama kwa watu wale wa vijiji nilivyovisema.

Mheshimiwa Spika, maji kama walivyosema wenzangu, mimi Wananchi wa Ileje wamenikataza kusema kama alivyosema fulani, lakini niseme kwamba, ninavyofahamu maji ni kila kitu. Mama anapokwenda kuchota maji kilomita tano, akifika kule anakuta foleni wenzake wamewahi, anaweka debe lake au ndoo yake, anaanza kusubiri saa kumi na moja alfajiri, zamu yake ya kuchota maji inakuwa saa tatu asubuhi, akirudi nyumbani muda wa kwenda shambani umekwisha. Uchumi hauwezi kwenda kwa njia hiyo, maji ni kila kitu, maji hospitalini hakuna operesheni bila maji, hakuna kunywa dawa bila maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi hauwezi kwenda bila maji. Nasisitiza sana; Wananchi wa Isongole wanashindwa kufanya kazi hasa akina mama na ninashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ninamwona, roho zinawasiliana kwamba ananisikiliza. Naomba shilingi milioni 500 kwa ajili ya Isongole.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu lengo langu lilikuwa kulia kwa ajili ya Isongole, niwape nafasi wachangiaji wengine. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa yale niliyotendewa katika Wilaya ya Ileje, kwa mara ya kwanza, Vijiji vya Ilanga, Miradi inaendelea, nimeambiwa pesa imefika Ikumbilo na Chitete. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa nitofautiane na wenzangu kwa kuunga mkono hoja. Ninaunga mkono hoja hii nikitegemea hautanipita na mimi katika nyongeza ambayo Serikali itajipapasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwanzoni tu baada ya maswali, kulikuwa kuna mtu aliomba mwongozo, Mheshimiwa Nchemba, kama ingewezekana kuendelea na mazungumzo katika hali iliyokuwepo. Toka jana mpaka leo,

ukweli ni kwamba, sisi tunaoangalia hakuna anayeunga mkono suala hili zima.

Pia mkumbuke kwamba, utaratibu tuliojianzishia sisi wenyewe, upo utaratibu wa mashauriano, tunashauriana katika *bracket* hiyohiyo, Bajeti ya Serikali kama ilivyowekwa katika *framework,* lakini tunaweza kupitia Kamati ya Bajeti kuangalia. Pamoja na shutuma zote anazopewa Spika kwa Kamati ya Bajeti, jamani mpaka tumefikia mfumo huu, haikuwa rahisi, kulikuwa na ubishi, woga, hofu na kila kitu, bahati nzuri mimi nilishajaribu, maji niliyaribu.

Kipindi kilichopita, bajeti ya mwaka jana, nilikuwa nimetumia fedha za *Legislative Support Program* ya Bunge. Waliotupa pesa zile walikuwa wanasema tuwe tunakwenda Majimboni, nikasema kwenda Majimboni, Majimbo yapo 239 huwezi kutumia dola milioni 3,500,000 zikatumika kwa Majimbo kwa miaka mitano ambayo ni kudanganya toto. Tukasema tufanye kitu kimoja, tuunde Kamati ndogo tuangalie hivi kweli Serikali imeshindwa kukusanya mapato katika maeneo fulani? Bahati nzuri Kamati ile ilifanya kazi bila kujitangaza kisiasa. Imesaidia sana kuona kwamba, tunaweza kufungua mahali pengine pa kukusanya kodi na Mwenyekiti wake alikuwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi wakati ule, Mheshimiwa Chenge.

Sasa mtu kama mimi, watu wana hofu ya mabadiliko na kila kitu, nimetumia kifungu changu cha tano kumteua Mwenyekiti wa *Budget Committee,* sijavunja sheria wala sijavunja demokrasia ila nilitaka nijihakikishie kwamba kazi ninayofanya kweli inazaa matunda. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, sasa naiona kabisa *call* ya Wabunge wote na ninadhani na Wananchi wote wanaotusikiliza, suala la maji hatuwezi kufanya utani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naitaka Kamati ya Bajeti na Serikali kwa maana ya Hazina na Wizara ya Maji na Kamati ya Sekta, naahirisha Bunge sasa hivi wakafanye kazi na kazi hii tutaimaliza Siku ya Jumatatu. Kwa hiyo, Siku ya Jumatatu

tuweze kupata maelezo kamili kama zimeongezeka basi zimeongezeka vipi na *addendum* inakuwaje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.33 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 29 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*